


**Vichanga na wagonjwa wafa kwa kukosa oksijeni**




**Kwa nini unahitaji kuvaa Kawaida?**




**Hii kauli ya Lema ina ukakasi mkubwa**

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo




| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00038 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Novemba 15 - 21, 2023 |

# Dk. Tulia: Samia mfano wa kuigwa



**Jamii inapaswa kuondoa fikra potofu kwamba wanawake hawapendani na badala yake waige mfano wa Rais Dk. Samia kwa namna anavyojitoa kwa kuwapambania na kuwapa nafasi wanawake wenzake katika nyadhifa mbalimbali za uongozi.**






## Waziri Ummy atoa siku saba apewe ripoti kifo cha mjamzito, kichanga




## Bashungwa aagiza ujenzi wa barabara Kimara-Bonyokwa uanze haraka

## Biteko aagiza vigogo Tanesco na TPDC wasimamishwe

Uk.4



## Mchakato Hadhi Maalum kwa diaspora kukamilika mwakani

Uk. 3

## Wizara ya Afya 'yapigwa jeki' vifaa vya maabara

Uk. 2

## CCM na CPV kunufaisha sekta ya uzalishaji

Uk. 3

# Bashungwa aagiza ujenzi barabara Kimara-Bonyokwa uanze haraka

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, wametembelea barabara ya Kikwete Highway itokayo Kimara Mwisho kuelekea Bonyokwa kuangalia changamoto zinazowakabili watumiaji hususani katika kipindi hiki cha mvua ambacho kimechangia uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara.

Wananchi walijitokeza kwa wingi kuelezea kero na changamoto wanazopata zikiwemo kukosa huduma ya afya, nauli za bajaj na bodaboda kupanda, biashara zao kukwama na zaidi kila mwaka wanapewa ahadi wanapohitaji utatuzi wa changamoto zao.

Waziri Bashungwa aliwahakikishia wananchi wa maeneo hayo kwamba mkandarasi anatakiwa kuanza ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita saba kwa kiwango cha lami mwezi ujao na kwamba ameagiza ujenzi wa dharura uanze mara moja.

"Ninakuelekeza Meneja Tanroads gusa mfuko wako wa dharura tafuta mkandarasi ambaye wakati wananchi wamelala yeye anatengeneza hii barabara," alisema Waziri Bashungwa.

Kwa upande wake, Chalamila alitilia mkazo suala la ujenzi huo uanze muda huo huo kwa kumuagiza Meneja wa Tanroads abaki pale kuanza kazi na kuahidi kufika kukagua na kuwachukulia hatua iwapo hawatafuata maelekezo waliyopewa.

"Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema wakatafute pesa ya dharura, nataka niwaahidi kesho jioni (jana), saa mbili ya usiku nitakuwa hapa," alisema RC Chalamila.

Vilevile, Chalamila aliwataka watumie 'molam' ili kuepuka utelezi kwa watumiaji, ni muhimu kurudisha mawasiliano kati ya pande hizo mbili, matatizo wanayokumbana nayo ni makubwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, bado ana mipango mingi ya utoaji wa fedha ili kuendelea kutatua kero za muda mrefu na zile za muda mfupi kwa wananchi.



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa.

Naye mbunge wa Jimbo hilo la Ubungo Profesa Kitila Mkumbo alisema kwamba wananchi wanapokuwa na shida, wana haki ya kuwalaumu viongozi wao na kuwaomba wawe na subira kwa kuwa barabara hiyo imeshaingia kwenye mpango na suala hilo lishafika bungeni na ipo kwenye bajeti.

Awali, Waziri Bashungwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Chalamila, walifanya ziara Kata ya Kibamba na kukagua ujenzi wa barabara inayoanzia Kibamba Shule kuelekea Mpiji Magohe yenye urefu wa kilomita 9.2 ambapo tayari zimekamilika kilomita mbili huku kilomita 1.5 ujenzi wake unaendelea. Sambamba na hapo, walifika mpaka Kiluvya kukagua mchakato wa ujenzi wa barabara ya mwendokasi inayotarajiwa kufika Kibaha.

# Wizara ya Afya `yapigwa jeki' vifaa vya maabara

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya, imepokea msaada wa vifaa vya maabara vyenye thamani ya zaidi ya Dola za Kimarekani 488,000 ili kusaidia upimaji wa vimelea vya malaria na magonjwa mengine kwa ufanisi zaidi ikiwa ni mpango wa Rais wa Marekani wa kupambana na ugonjwa huo (PMI).

Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUCOHAS), kimekabidhiwa sehemu ya msaada huo kwa niaba ya vyuo vilivyopo chini ya Wizara ya Afya vinavyotoa mafunzo ya kozi ya maabara vilivyopo katika mikoa sita vitakavyofaidika na msaada huo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Anne Murphy, Mkurugenzi wa Ofisi ya Afya kutoka USAID Tanzania, alisema kuwa hadubini 133 na vitendanishi vingine vya maabara vilivyotolewa, vitawezesha Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kuimarisha uwezo wa kimaabara katika uchunguzi na kusaidia utoaji matibabu ipasavyo na hivyo kusaidia kuokoa maisha ya watu na kuzuia madhara ya malaria.



Prof. Mohamed Janabi

> **Awali, akitoa salamu za ufunguzi, Mkurugenzi Hospitali ya Taifa Muhimbili...**

Serikali ya Marekani imeipongeza Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya kutokana na juhudi zake zilizosaidia kushuka kiwango cha ugonjwa huo nchini kutoka asilimia 14 mwaka 2015 mpaka asilimia nane mwaka jana.

Awali, akitoa salamu za ufunguzi, Mkurugenzi Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi, alishukuru kwa msaada huo uliolenga kusaidia kuendelea kupambana na kuutokomeza ugonjwa wa malaria nchini.

Aliongeza kuwa msaada huo umekuja wakati mwafaka kipindi ambacho serikali kupitia Wizara ya Afya imewekeza fedha nyingi ili kuboresha huduma za afya nchini kwa kununua dawa na vifaa tiba.

# Uwekezaji PSSSF wafikia tril. 8.6/-




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimkabidhi cheti cha shukrani, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama wa PSSSF, James Mlowe (kushoto) jijini Lindi jana. (Picha: Khalfan Said).

**Na Mwandishi Wetu, Lindi**

MFUKO wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), hadi kufikia Septemba, mwaka huu, umewekeza zaidi ya Sh. trilioni 8.6 hadi kufikia Septemba,mwaka huu.

Hayo yalisemwa na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama PSSSF, James Mlowe, alipokuwsa akitoa elimu ya Hifadhi ya Jamii kwa Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Saba wa Jukwaa la Wahariri Tanzanai (TEF) mjini Lindi jana.

Mlowe alisema mafanikio hayo ya uwekezaji ni ya kujivunia kwani ni makubwa ndani ya kwa kiasi kikubwa na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za kuongeza ajira, kufungua nchi na kuboresha mazingira ya uwekezaji.

Kwa upande wake, Meneja Mafao wa PSSSF, Ramadhani Mkeyenge, alisema ukiacha jukumu hilo la Mfuko katika eneo la uwekezaji, pia umetekeleza kwa mafanikio makubwa jukumu la Ulipaji Mafao.

Alisema Mfuko unatoa jumla ya mafaosaba ambayo ni pamoja na Fao la Uzeeni (Pensheni), Fao la Ulemavu, Fao la Kifo, Fao la Urithi, Fao la Uzazi, Fao la Kukosa Ajira na Fao la Ugonjwa. Mfuko unalipa pensheni kwa wastaafu 167, 937 na wategemezi, wastani wa Sh. bilioni 67 kila mwezi." alifafanua Mkeyenge

"Mfuko tangu uanze kutekeleza majukumu yake mwaka 2018 hadi Juni 2023, umelipa kiasi cha Sh. trilioni 8.8 kwa wanachama wapatao 262,095," alisema na kuongeza kua kila mwezi pensheni inayolipwa kwa wastaafu na wategemezi ni wastani wa Sh. bilioni 67.



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, akizungumza na ujumbe wa Kamati Kuu ya chama cha CPV cha Vietnam uliongozwa na Profesa Le Hai Binh, katika Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya CCM, Lumumba, jijini Dar es Salaam juzi.

# CCM na CPV kunufaisha sekta ya uzalishaji

**Na Godfrey Sanga**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema chama hicho kinaridhishwa na urafiki na uhusiano wake na Chama cha Kikomunisti cha Vietnam (CPV), na kipo tayari kuendeleza ushirikiano kati yao utakaoongeza fursa kwa Tanzania kunufaika zaidi katika sayansi na teknolojia, kukuza uzalishaji na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, maeneo ambayo Vietnam ina uzoefu mkubwa.

Katika taarifa iliyotolewa na mtandao wa kijamii wa Instagram ya CCM jana, Chongolo alisema kupitia uhusiano wa kihistoria uliopo kati ya CCM na CPV, kisiasa, kijamii na kiuchumi, vyama hivyo vitaimarisha zaidi misingi itakayotumiwa na Serikali za nchi zote mbili kubadilishana uzoefu na mikakati sahihi ya kubadili hali za maisha ya watu, kupitia sekta ya uzalishaji, ambayo ni hatua muhimu katika ukuaji wa uchumi wa taifa.

Aliyasema hayo alipokutana na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CPV, Profesa Le Hai Binh, mapema jana kwenye mazungumzo ya kikazi yaliyofanyika Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya CCM, Lumumba, jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wake, Prof. Le Hai Binh, alisema thamani ya CCM, Serikali yake na Tanzania kwa ujumla mbele ya CPV na Vietnam, ni kubwa mno, kwa sababu za kihistoria, ambapo vyama hivyo na nchi zote mbili, zina mtazamo mmoja wa itikadi ya kisiasa na kiuchumin na historia imewapitisha katika ushirikiano wa mapambano ya watu wanyonge kujikomboa.



## Mchakato Hadhi Maalum kwa diaspora kukamilika mwakani

**Na Mwansishi Wetu**

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imesema inatarajia kukamilisha utaratibu wa kuwapatia Hadhi Maalum Watanzania waishio nje ya nchi (diaspora) ifikapo mwakani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kupitia mtandao wa Instagram wa wizara hiyo baada ya kikao cha hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na diaspora wa Tanzania nchini Uholanzi kwa heshima ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, ambaye yupo nchini humo kwa ziara ya kikazi ya siku tatu inayomalizika leo, utaratibu huo utakamilika mwakani.

Akifafanua masuala mbalimbali yaliyowasilishwa kupitia risala ya Watanzania iliyosomwa na mwakilishi wa Umoja wa Watanzania waishio nchini Uholanzi, Sylvana Lubuva, Waziri Makamba alisema utekelezaji wa Hadhi Maalum unategemea kufanyika kwa mapitio ya baadhi ya sheria za nchi kama ile ya ardhi na uhamiaji ili kurahisisha utekelezaji wenye tija kwa walengwa, yaani diaspora na kwamba mchakato huo unatajiwa kukamilika kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/24.

"Miongoni mwa masuala yatakayopewa kipaumbele kwenye Hadhi Maalum ni haki ya kurithi au kurithishwa mali kwa diaspora wa Kitanzania aishiye nje ya nchi...ili kutekeleza hili kuna maeneo ya sheria yetu lazima yabadilishwe ili watoto wenu wanaoishi huku nje waweze kurithi au kumiliki ardhi," alisema.

Kuhusu utaratibu wa kulipa viza pindi diaspora wanaporudi nyumbani alisema wataruhusiwa kuja nyumbani na kukaa kwa muda wanaotaka bila malipo ya viza.

Hata hivyo, alisema ili hilo litekelezwe, lazima Sheria ya Uhamiaji ipitiwe na kurekebishwa ili kuruhusu kurudi nyumbani bila kulipishwa viza.

Alisema baadhi ya masuala mengine yatakayowanufaisha watumiaji wa Hadhi Maalum ni fursa na motisha mbalimbali za kuwekeza nchini Tanzania kupitia Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC).

Kadhalika, Makamba alisisitiza umuhimu wa kujisajili kwenye mfumo wa Diaspora Digital Hub ambapo alisema licha ya kusaidia kuwatambua Watanzania waishio nje ya nchi, pia inarahisisha kwa kiasi kikubwa kuwarejesha nchini pindi majanga makubwa yanapotokea maeneo mbalimbali duniani.

**Miongoni mwa masuala yatakayopewa kipaumbele kwenye Hadhi Maalum ni haki ya kurithi au kurithishwa mali kwa diaspora wa Kitanzania aishiye nje ya nchi...ili kutekeleza hili kuna maeneo ya sheria yetu lazima yabadilishwe ili watoto wenu wanaoishi huku nje waweze kurithi au kumiliki ardhi.**

# Dk. Tulia: Samia mfano wa kuigwa

**Na Mwandishi Wetu**



SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Dk. Tulia Ackson, amesema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ni mfano wa kuigwa katika kupambania na kuwapa wanawake fursa za uongozi.

Aliyasema hayo katika hafla ya kumpongeza kwa ushindi wa Urais wa IPU iliyoandaliwa na Chama cha Walimu Wilaya ya Mbeya jana.

"Jamii inapaswa kuondoa fikra potofu kwamba wanawake hawapendani na badala yake waige mfano wa Rais Dk. Samia kwa namna anavyojitoa kwa kuwapambania na kuwapa nafasi wanawake wenzake katika nyadhifa mbalimbali za uongozi," alisema.

Alimshukuru Rais Dk. Samia kwa namna alivyohakikisha Tanzania inashinda katika uchaguzi wa IPU kwa kuwa nafasi hiyo ilikuwa ni lazima nchi husika itoe ridhaa ya kutoa mwakilishi na kwa upendo wake alifanya hivyo.

Alisema kuchaguliwa kwake pamoja na mambo mengine kumechangiwa na uongozi shupavu wa Rais Samia ambaye ameimarisha diplomasia ya kimataifa na kufanya watu wengi waizungumze Tanzania vizuri.

Katika uchaguzi wa Rais wa IPU uliofanyika jijini Luanda nchini Angola Oktoba 27, mwaka huu wakati wa Mkutano wa 147 wa Umoja huo, Dk. Tulia alipata kura 172 sawa na asilimia 57 ya kura 303 zilizopigwa na wajumbe walioshiriki mkutano huo.

Tulia aliwashinda wagombea wengine watatu, Adji Diarra kutoka Bunge la Senegal aliyepata kura 59, Catherine Hara, Spika wa Bunge la Malawi aliyepata kura 61 na Marwa Hagi kutoka Bunge la Somalia, aliyepata kura 11.

Katika hafla ya Chama Cha Walimu (CWT) Wilaya ya Mbeya ya kumpongeza Dk. Tulia, aliwataka walimu wote nchini kuendelea kuweka juhudi katika kujenga taifa lililoelimika kwa kutoa elimu iliyo bora kwa wanafunzi.

Alisema serikali imefanya kazi kubwa kwa kuboresha mazingira ya kazi na kuwa rafiki ikiwemo kulipwa madai yao mbalimbali na kwa wakati.

# Waziri Ummy atoa siku saba apewe ripoti kifo cha mjamzito, kuchanga

**Na Mwandishi Wetu, Tanga**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ametoa maelekezo kwa Baraza la MadaktaribTanganyika (MCT) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (TNMC), kuhakikisha ndani ya siku sab wamempelekea taarifa ya tukio la kifo cha mjamzito na kichanga chake kilichotokeaNovemba 11, mwaka huu mkoani Tanga.

Amesema tayari hatua za awali zimeshachukuliwa ikiwemo ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba, kutuma timu kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa inayojumuisha Madaktari Bingwa wawili akiwemo Daktari Bingwa wa Wanawake na Uzazi na Daktari Bingwa wa Huduma za Usingizi kufanya uchunguzi wa tukio hilo.

"Hatua nyingine iliyochukuliwa baada ya tukio hilo, ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, kuwasimamisha kazi watumishi watatu walioshiriki kumpatia huduma mjamzito huyo tangu alipopokelewa kituoni hadi umauti ulipomkuta ili kupisha uchunguzi wa tukio hilo baya na lisilopaswa kuvumiliwa," alisema Waziri Ummy.

Aidha, Waziri Ummy amewahakikishia Watanzania kuwa baada ya kupokea taarifa ya uchunguzi, kila mtumishi aliyehusika atachukuliwa hatua kali za kitaaluma, kiutumishi na kijinai ikiwemo kufikishwa mahakamani kujibu tuhuma za kijinai pale itakapothibitika.

Wakati huo huo, Waziri Ummy ametoa pole kwa familia iliyoguswa na msiba huo na ameahidi kuwa serikali kupitia Wizara ya Afya itaendelea kusimamia ubora wa huduma za afya ili kufikia matarajio ya wananchi wote.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.

# Radi yaua mmoja, ng'ombe 27 Sumbawanga

**Na Mwandishi Wetu**

MTU mmoja amefariki dunia na ng'ombe 27 wamekufa baada ya kupigwa na radi katika maeneo na muda tofauti wilayani Sumbawanga.

Katika Kijiji cha Muze, mkulima Edward Ibrahim Silungu (32), alifariki dunia papo hapo na ng'ombe wawili aliowatumia kulima shamba wakati mvua zikinyesha kufa.

> **Alisema radi ilimpiga kijana wake ambaye alifariki dunia papo hapo na ng'ombe...**

Tukio kama hilo limeripotiwa kutokea katika Kijiji cha Tamasenga baada ya ng'ombe 25 kupigwa na radi na kufa.

Baba mzazi wa kijana aliyefariki dunia, Ibrahim Silingu alisema walikuwa shambani wakiendelea na kilimo ndipo mvua zikaanza kunyesha na baada ya muda mfupi, wakasikia ngurumo zilizoambatana na radi.

Alisema radi ilimpiga kijana wake ambaye alifariki dunia papo hapo na ng'ombe wawili waliowatumia kwa kilimo nao walikufa.

Akizungumzia matukio hayo, Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Ally Chirukile amewataka wananchi kuchukua tahadhari katika kipindi hiki cha mvua kubwa ikiwa ni pamoja na kuacha kufanya shughuli za kilimo kwa kutumia ng'ombe wakati mvua zikiendelea.

# Biteko aagiza vigogo Tanesco na TPDC wasimamishwe kazi

**Na Mwandishi Wetu, Mtwara**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), kumsimamisha kazi Meneja wa Huduma kwa Wateja kwenye shirika hilo na kuweka mtu mwingine kufanya hiyo kazi.

Pia amemuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), kumuondoa mara moja kazini Ofisa Uhusiano na kuweka mtu mwingine kwa kushindwa kufanya kazi yake.

Biteko alitoa maagizo hayo jana wakati akizungumza na wananchi katika Kijiji cha Msimbati Halmashauri ya Mtwara.

Alisema Meneja wa Huduma kwa Wateja Tanesco, amekuwa akitoa majibu yasiyoridhisha kwa wateja pindi wanapopiga simu kwenye shirika kupata majibu kutokana na tatizo la umeme.

"Tanesco tuna kitengo cha Huduma kwa Mteja , ni kweli tuna changamoto ya umeme, lakini watu wakipiga simu, majibu wanayojibiwa wananiandikia meseji, wakilalamika majibu wanayopewa siyo yenyewe," alisema.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko.

Dk. Biteko aliyeonkana kukerwa na mwenendo wa Meneja huyo wa Huduma kwa Wateja, alisema ni lazima watendaji serikalini wawajibike ipasavyo.

"Nimemuelekeza Mkurugenzi wa Tanesco yule Meneja wa Huduma kwa Wateja pale Tanesco, omundoa mara moja na kumweka mtu mwingine," alisema na kuongeza:

"Lazima tuheshimiane kazi ifanyaike, wananchi wanataka umeme, watu wanataka gesi, watu wanataka gesi ibadilishe maisha yao, hatuwezi kuja hapa tumevaa tumependeza, watu wanalia shida ndogo ndogo," alisema.

Kwa upande wa Ofisa Uhusiano TPDC, Biteko alisema ameshindwa kufanya kazi yake ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa na , kusikiliza kero kwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya miradi ya gesi nchini.

# 37 wachukua fomu kuwania Uenyekiti

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

MAKADA 37 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mwanza, wamejitokeza kuchukua fomu za kuwania Uenyekiti wa mkoa huo baada ya nafasi hiyo kuwa wazi kutokana na aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama wa mkoa huo, Sixbert Jichubu, kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Masasi.

Katibu wa CCM Mkoa wa Mwanza,, Omari Mtuwa, aliyasema hayo juzi na kuongeza kuwa idadi hiyo inatokana na uwapo wa demokrasia ndani ya Chama. "Tangu fomu zianze kutolewa Novemba 12, mwaka huu, hadi sasa idadi ya waliochukua fomu ni 37 na tunatarajia itaongezeka, hii ni kutokana na demokrasia iliyoimarika ndani ya Chama chetu," alisema.

Baadhi ya makada waliochukua fomu kuwania nafasi hiyo ni aliyekuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi CCM Mkoa wa Mwanza, Simon Mayunga, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Misungwi, Michael Smart na Mwenyeki wa CCM Wilaya ya Sengerema, Marco Makoye.

**Tangu fomu zianze kutolewa Novemba 12, mwaka huu, hadi sasa idadi ya waliochukua fomu ni 37 na tunatarajia itaongezeka, hii ni kutokana na demokrasia iliyoimarika ndani ya Chama chetu.**



**Afisa Utumishi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini(Ruwasa)Mkoa wa Songwe, Bahati Nyamadyaki, kushoto, akimtua ndoo ya maji mkazi wa Kijiji cha Maheche Wilaya ya Ileje mkoani humo, Sarah Mayola, baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi wa maji safi na salama wa Ntembo -Msia uliotekelezwa na Ruwasa kwa gharama ya Sh. milioni 455. (Picha: Mpigapicha Wetu)**

# Raia wa kigeni adakwa akisafirisha mirungi

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

JESHI la Polisi mkoani Arusha, limewakamata watuhumiwa 188 akiwemo raia mmoja wa nchi jirani kwa tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Salvas Makweli, alisema watuhumiwa wawili kati yao, walikamatwa wakiwa na bunda 542 zenye kilo 298 zinazodaiwa kuwa dawa za kulevya.

Aliwataja watuhumiwa hao waliokamatwa eneo la Philips jijini hapa kuwa ni Gilbert Joseph (33), mkazi wa Sinoni na Peter Waweru (33), mkazi wa nchi jirani wakiwa wanasafirisha dawa hiyo kwa lori aina ya Isuzu.

Akizungumza na vyombo vya habari jana, Makweli alisema jeshi hilo lilifanya operesheni maalumu kuanzia Oktoba 13 hadi Novemba 13, mwaka huu kwa lengo la kuwakamata watuhumiwa wanaojihusisha na matukio ya uhalifu.

Alisema Novemba 12, mwaka huu, saa 3:00 asubuhi, eneo la Philips katika Halmashauri ya Jiji la Arusha walifanikiwa kumkamata Gilbert Joseph (33) mkazi wa Sinoni jijini hapa na Peter Waweru (33), mkazi wa nchi jirani (hakutaja nchi hiyo) wakiwa wanasafirisha dawa za kulevya aina ya mirungi bunda 542 zenye uzito wa kilo 298 kwa kutumia gari aina ya Isuzu (namba zimehifadhiwa). Kaimu Kamanda Makweli alisema watuhumiwa wote wawili wanaendelea kuhojiwa na kwamba upelelezi utakapokamilika jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.




**Na Mwalimu Paul Masatu | Simu: 0766 775 255**

# Ushindi wowote huanzia ndani yako




Mara nyingi watu tumeongelea maisha ya ushindi kwamba ni kitu au mafanikio yanayoonekana mbele za watu. Wanadhani ushindi ni ule ambao watu wanauona na ule unaokuletea sifa.

Lakini ukweli ni kwamba, ushindi wowote mkubwa na wa kudumu unaanzia ndani yako. Vita unaishinda kwanza ndani ndipo ushindi unaanza kuonekana nje hatua kwa hatua.

Ushindi huu unajengwa ndani yako kuanzia kwenye maarifa unayoyapata, mtazamo, nguvu ya maamuzi, kuchukua hatua, ustahimilivu (kutokatishwa tamaa), machaguo yako kwenye maisha ya kawaida, tabia (character), kujijengea uwezo, vipawa, aina za marafiki unaojitengenezea, n.k.

Haya yote ukiyatazama, yanaanzia ndani. Maisha yamejaa vita nyingi na uwanja wa vita ni akili yako. Mtu ambaye tunamwona ana mafanikio, ni yule ambaye vita za ndani yake anazishinda nyingi kuliko zile anazopoteza.

Mfano, vita vinaanza asubuhi kitandani kwenye kuamua je, nilale kidogo au niamke nikatekeleze malengo? Vita nyingine ni kwenye kutekeleza yake unayoyajua kama vile ambavyo unajua mazoezi ni muhimu, lakini unashindwa, unajua kuwa kuomba Mungu ni muhimu, lakini unashindwa, unajua kuwa kuweka akiba ni muhimu lakini unashindwa, unajua kwamba kutoa zaka, sadaka na kuwa mkarimu kuna baraka, lakini unashindwa na mambo mengine mengi yanayofanana na hayo. Sasa kushindwa huku kwingi ndiyo vikwazo vya kufanikiwa kwa watu wengi.

Usipojizoeza kushinda vikwazo na mitihani kwenye maisha yako ya kibinafsi (private life) ni ngumu kuja kupata ushindi huku nje kwenye (kwenye public life). Hiyo ni kanuni ya mchakato (the law of process) huwezi kuivunja, ni kama mtoto hawezi kukimbia kabla ya kupitia hatua ya kutambaa.

Kwa wasomaji wa Biblia, wataona kabla ya Daudi kumuua Goliath waziwazi mbele ya maelfu ya watu na kupata promotion ya kuwa Mfalme, alianza kwanza na ushindi binafsi (private victories) kama vile kuua Dubu na Simba tena akiwa peke yake porini bila ya mtu yoyote kuona.

Kama tu usingizi na godoro vinakushinda huko chumbani kwako, unashidwa kuamka mapema, unashindwa hata kupangilia mambo yako, nitakuwa ngumu kuja kuzishinda changamoto zinazotokana na mahusiano ya watu huku nje.

Kama tu unashidwa kulimudu tumbo lako na kuidhibiti "appetite" yako, kama unashidwa kujizuia, je unafikiri utaweza kuwamudu washindani wako (competitors) huku kwenye soko (market place)?

Maisha ni mchakato (process), hivyo jitihada zozote za kutafuta mafanikio kwa njia za mkato (shortcuts), haziwezi kukupa ushindi utakaodumu.

Wework Consult
Your Partner in Growth.

# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi


## HII NI KERO

### Kujichukulia sheria mkononi



KUSHAMIRI kwa vitendo vya kujichukulia sheria mkononi dhidi ya watuhumkiwa wa uhalifu katika matukio mbalimbali kama vile ya wizi, kuwakamata, kuwapiga na kuwasababishia majeraha, wakati mwingine hata kifo, si jambo la kiungwana.

Ni muhimu kuripoti polisi pale matukio au watuhumiwa hao wanapokmatwa ili sheria ichukue mkondo wake.




MAONI YA MHARIRI

## Tupambane tumalize malaria

SERIKALI ya Marekani imeipongeza nchi yetu kutokana na juhudi zilizosaidia kushusha kiwango cha ugonjwa wa malaria kutoka asilimia 14 mwaka 2015 mpaka asilimia nane mwaka jana.

Pongezi hizo zilitolewa jana wakati Wizara ya Afya, ikipokea msaada wa vifaa vya maabara kutoka Mpango wa Rais wa Marekani wa kupambana na malaria (PMI).

Akizungumza katika hafla hiyo, Anne Murphy, Mkurugenzi wa Ofisi ya Afya wa Shirika la Misaada la Marekani, (USAID Tanzania), alisema vifaa hivyo ni darubini 133 pamoja na vitendanishi vingine vya maabara, vyote vikiwa na thamani ya Dola za Marekani 488,000.

Alisema vitasaidia kuimarisha Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kwa kuboresha uwezo wa kimaabara katika uchunguzi na kusaidia utoaji wa matibabu. Tunaipongeza Marekani kwa msaada huo huku pia tukijipongeza kwa hatua tuliyofikia katika kudhibiti maambukizi ya malaria nchini.

Hata hivyo, bado tuna kibarua cha kutokomeza kabisa malaria kwani zipo nchi kadhaa zilizofanikiwa katika hilo zikiwemo za Afrika kama Algeria, Lesotho, Morocco, Mauritius na Seychelles. Kama wao wameweza hata sisi tunaweza!

Takwimu za Shirika la Afya Duniani zinaonesha kwamba mwaka 2020 kulikuwa na wagonjwa wa malaria takribani milioni 241 na vifo 672,000 vilivyotokana na ugonjwa huo duniani kote.

Katika muktadha huo, malaria inabaki kuwa ugonjwa hatari kwani kama haupati tiba sahihi, unahatarisha maisha. Malaria huweza kusababisha matatizo ya kupumua, mimba kuharibika, ini na figo kushindwa kufanya kazi, pamoja na matatizo ya ubongo na mfumo wa neva.

Malaria pia ina madhara katika uchumi ikiwa ni pamoja na gharama za matibabu, kumfanya mgonjwa kushindwa kufanya kazi za uzalishaji mali na pia huweza kuogopesha watalii kutembelea nchi yetu wakihofia kuugua ugonjwa huo.

Wakati serikali ikipambana katika kudhibiti malaria, wananchi tusibweteke. Tufanye yale yanayosaidia kujikinga dhidi ya malaria. Mambo hayo ni pamoja na kutumia vyandarua na dawa za kuulia mbu kwa sababu mbu wanaosambaza ugonjwa huo kutoka kwa mwanadamu ambaye tayari ana maambukizi, huuma usiku.

Tunatakiwa kuharibu mazalia ya mbu kwa kufukia madimbwi na maeneo yote yanayotuamisha maji pamoja na kukata nyasi ndefu kwenye maeneo ya makazi yetu.

Ukisikia dalili za malaria kama vile homa, maumivu ya tumbo, uchovu, kichefuchefu, ugumu wa kupumua na kupoteza hamu ya kula, nenda ukapime kwenye kituo cha afya ili kuhakikisha kama ni malaria. Kama ni yenyewe tumia dawa kwa maagizo ya daktari.

Kwa kufanya hivyo, licha ya kujilinda na ugonjwa huu hatari, tutakuwa pia tunasaidia kumaliza kabisa malaria nchini. Tanzania bila malaria inawezekana.


## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255787559090
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com





Na Godfrey Sanga
JICHO LANGU
Sangagodfrey26@gmail.com


## Uwajibikaji hujenga jamii imara yenye maendeleo

WAJIBU ni kazi au jambo fulani ambalo ni lazima ufanye au kutimiza na hii inaweza kuwa kila siku au siku kadhaa. Kila mtu ana wajibu wake, tena muhimu kutambua wajibu unaokupasa kwani ni sehemu ya haki yako pia.

Mfano rahisi wa uwajibikaji ni wa baba kulinda familia yake, kusomesha watoto wake, kufanya kazi kwa bidii. Mama kumsaidia baba kazi, kuwapa watoto upendo, kwani mama ndiye anayekaa na watoto kwa muda mwingi kuliko baba. Na kwa upande wa mtoto anapaswa kutii wazazi, kufanya kazi za nyumbani na kusoma kwa bidii.

Hivyo basi jambo ambalo linahitajika kwa kila mmoja wetu kuchukua hatua na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na uadilifu

Kwa sasa, kuna changamoto nyingi katika utekelezaji na uwajibikaji katika maeneo mbalimbali, na hivyo kuna haja ya kuangalia jinsi wananchi wanavyoweza kuchangia na kufanya uchambuzi wa viwango vya uwajibikaji katika sekta tofauti.

Jicho langu leo linatoa hoja ya kwa nini uwajibikaji ni muhimu kwa maendeleo ya jamii na kuonyesha jinsi wananchi wanavyoweza kuchangia katika kuhakikisha viwango vya uwajibikaji vinazingatiwa katika sekta tofauti mahali popote pale.

Kuna umuhimu mkubwa sana katika uwajibikaji kwani huimarisha uhusiano wetu binafsi, kama vile kuwajibika kwa familia na marafiki pia.

Suala la uwajibikaji hupelekea matumizi bora ya rasilimali za umma kwa manufaa ya wananchi wote. Lakini, nchini uwajibikaji unakabiliwa na changamoto nyingi, hasa katika baadhi ya sekta za serikali, biashara, na mashirika ya kijamii. Uwazi na ukweli ni muhimu ili kuzuia matumizi mabaya ya mamlaka, ufisadi, na ubadhirifu wa rasilimali za umma.

Ni muhimu kwa serikali, biashara, na mashirika ya kijamii kutekeleza mifumo madhubuti ya uwajibikaji ili kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa njia sahihi. Kwa kufanya hivyo, tunaweza kujenga nchi yenye uwajibikaji na maendeleo endelevu.

Kuna hatua kadhaa za kuboresha uwajibikaji katika jamii. Kwanza, kuhamasisha uelewa wa umma kupitia elimu ya umma. Pili, serikali inaweza kuweka sheria kali na kuunda taasisi za kusimamia utekelezaji wa sheria hizo.

Kukuza uwazi katika taasisi za umma na kuhimiza utendaji wa uwajibikaji pia ni muhimu. Kwa mujibu wa ripoti iliyowahi kutolewa na mashirika ya kimataifa na balozi mbalimbali katika mada ya uwajibikaji waliwahi kugusia na kusema, "nchi kama Norway, Uswisi, na Singapore zimefanikiwa katika kuboresha uwajibikaji kupitia sheria kali, taasisi madhubuti, na juhudi za kuhamasisha uelewa wa umma na kukuza uwazi."

Ni ukweli usiopingika kuwa ushiriki wa wananchi ni muhimu sana katika kuboresha uwajibikaji katika jamii. Wananchi wanapaswa kuhusishwa katika michakato yote inayohusiana na maamuzi na utekelezaji wa sera za umma. Wananchi wanapaswa kuwa na sauti katika kufuatilia na kuchambua mipango na matumizi ya rasilimali za umma ili kuhakikisha uwazi na uwajibikaji.

Kutathmini uwajibikaji ni muhimu ili wananchi wapate huduma bora kutoka kwa serikali. Njia za kutathmini ni pamoja na ufuatiliaji wa sera na miradi, ukusanyaji wa maoni ya wananchi na tathmini ya utendaji wa watumishi wa umma. Hata hivyo, hali ya uwajibikaji nchini inaonekana kuwa duni.

Ni muhimu kuchukua hatua za haraka ili kuboresha tathmini ya uwajibikaji kama vile kuongeza uwazi na kuhusisha wananchi katika mchakato wa maamuzi. Pia inapaswa kuwepo mifumo bora ya ufuatiliaji na tathmini ya utendaji wa watumishi wa umma.

Ewe baba, mama, dada, kaka na jamii kwa ujumla suala la uwajibikaji ni la kila mmoja wetu licha ya kwamba wajibu huwa ni tofauti. Taifa lina jengwa kwa umoja wetu pia uwajibikaji ni muhimu katika kujenga jamii imara na yenye maendeleo.

Kazi Iendelee

# Kamati ya Bunge yaahidi makubwa kwa Dawasa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge, Uwekezaji na Mitaji ya Umma, imeahidi kuendelea kuisaidia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa) kupata fedha za kusambaza huduma ya majisafi kwa wananchi wa maeneo yote ya Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani.

Hayo yalisemwa Mwenyekiti wa Kamati, Deo Sangu walipotembelea utekelezaji wa mradi wa maji Chalinze awamu ya tatu unaohusisha upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji wa Wami.

Alisema Dawasa inafanya kazi kubwa ya kuhakikisha huduma ya majisafi inapatikana kwa wananchi wote kwa kutumia mapato ya makusanyo ya ndani.

Aliongeza kuwa miongoni mwa maazimio ambayo Kamati imetoa kwa serikali kwa ajili ya utekelezaji ni pamoja na kuhakikisha madeni ya taasisi za serikali zinazodaiwa na Dawasa zinalipwa ili kasi ya maboresho ya huduma za maji iendelee kwa kasi ili kuongeza nguvu katika utoaji wa huduma ya majisafi kwa wanachi wote.

"Pia na madeni ya maji ya taasisi yaweze kulipwa ili kazi ya kusambaza maji kwa wananchi kupitia miradi mikubwa kama huu wa Chalinze awamu ya tatu iweze kuleta tija kwa wananchi, tunaipongeza Menejimenti ya Dawasa kwa jitihada kubwa wanazofanya za kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi wote," alisema Mwenyekiti Sangu.

"Lengo la ziara ya Kamati hii ni kusimamia utekelezaji wa matumizi ya mitaji ya serikali kwa taasisi ili tija ya uwekezaji iweze kuonekana," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Aboubakar Kunenge, aliishukuru Kamati kwa kutembelea na kujionea jitihada zinazofanywa na Dawasa kwa kushirikiana na Mkoa katika kufanikisha azma ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani.

Alisema kuwa kwa sasa upatikanaji wa majisafi kwenye Mkoa wa Pwani ni asilimia 85, ongezeko linalovutia uwekezaji mkubwa wa viwanda.

Aliliomba Bunge kupitia Kamati kuiwezesha Dawasa kupata fedha zaidi za kusambaza maji kwa wananchi wote wanufaika wa miradi.

Naye Mbunge wa Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete, aliieleza Kamati kuhusu jitihada kubwa zilizofanywa na serikali kupitia Dawasa za kutekeleza mradi wa Chalinze awamu ya tatu pamoja na mradi wa maji Mlandizi - Chalinze - Mboga ambao umekamilika na umeleta unafuu a maji.

Naye Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Kiula Kingu, alisema kuwa mradi wa maji Chalinze ulipitia hatua mbalimbali za utekelezaji kuanzia awamu ya kwanza, ya pili na sasa awamu ya tatu ambayo inaendelea.

Alisema awamu hii ya tatu ambayo imegharimu bilioni 83, mradi unahusisha upanuzi wa uwezo wa Mtambo wa Wami kutoka uzalishaji wa lita milioni 7.2 kwa siku hadi lita milioni 21.6 kwa siku.

Aliongeza pia mradi umehusisha ujenzi wa matangi 18 ya kuhifadhi maji pamoja na ujenzi wa vioski 351 vya kuchotea maji ambavyo tayari vimekamilika.

"Mradi umelaza bomba la usamabazaji maji kwa umbali wa kilomita 826 na unalenga kunufaisha wakazi wa vijiji zaidi ya 56," alisema Kingu.

**kwa sasa upatikanaji wa majisafi kwenye Mkoa wa Pwani ni asilimia 85, ongezeko linalovutia uwekezaji mkubwa wa viwanda.**
**Ninaliomba Bunge kupitia Kamati kuiwezesha Dawasa kupata fedha zaidi za kusambaza maji kwa wananchi wote wanufaika wa miradi.**


Aboubakar Kunenge

# Vyombo vya habari vyatakiwa kutumia Kiswahili fasaha

**Lugha zinazotumika, ni mbovu na habari mpaka inaruka hewani au inachapishwa gazetini inapitia kwenye mikono mingi, lakini bado inatoka ikiwa na makosa ya kisanifu, hivyo wananchi wanalishwa habari zisizo stahili, tunawanoa waandishi hapa ili kuwajengea uwezo kisanifu.**


Dk. Egbert Mkoko

**Na Hellen Mwango, Dodoma**

MHADHIRI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Egbert Mkoko, amevishauri vyombo vya habari kutumia Kiswahili fasaha kwa habari zinazotangazwa katika redio, televisheni au kuchapishwa kwenye magazeti.

Aliyasema hayo jijini Dodoma jana wakati akiwasilisha mada katika mafunzo ya siku tatu ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuhusu umahiri wa habari za uchunguzi zinazohusu haki za binadamu.

"Lugha zinazotumika, ni mbovu na habari mpaka inaruka hewani au inachapishwa gazetini inapitia kwenye mikono mingi, lakini bado inatoka ikiwa na makosa ya kisanifu, hivyo wananchi wanalishwa habari zisizo stahili, tunawanoa waandishi hapa ili kuwajengea uwezo kisanifu.

"Waandishi tujinoe katika kutumia lugha ya Kiswahili fasaha katika kuhabarisha umma, pia tuache kuchukua upande mmoja wa habari zetu, tuzingatie usawa ili tuweze kuwalisha wananchi kilicho sahih," alisema.

Alisema hali ya uandishi kwa sasa, inasikitisha ikiwamo baadhi ya vyombo vya habari kuchapisha au kutangaza picha ambazo kimaadili ya uandishi zinatakiwa kuhifadhiwa kwa maslahi ya watoto/mtoto husika.

Kwa upande wake, Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu Kanda ya Afrika Mashariki, Catherine Njuguna, alitaka waandishi wa habari kuandika habari zenye tija kwa jamii huku wakizingatia haki za binadamu.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, alisema waandishi wa habari wanapaswa kufuata maadili na miongozo ili kuleta tija badala ya kuweka maslahi mbele katika kuandika habari za haki za binadamu.

Alisema lengo la MCT kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kuandaa mafunzo hayo wanalenga kuongeza uelewa kwa waandishi wa habari pamoja na kuelewa kuhusu usalama kwa waandishi kwa kufuata maadili ya uandishi wa habari bila upendeleo wowote.

"Vyombo vya usalama, vina wajibu wa kumlinda mwandishi wa habari kama mwananchi mwingine na kwa kupitia mafunzo hayo maalumu waandishi wa habari wa wataelewa kwa mapana kuhusu haki za binadamu na kuripoti," alisema.

# Dk. Tulia: Samia ni chachu ya maendeleo Mbeya

**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

ILIKUWA Jumamosi, Novemba 11, 2023, saa saba za mchana, umati wa wakazi wa Jiji la Mbeya waliposhuhudia binti yao, rafiki yao, dada yao, mwana-Mbeya mwenzao, mwakilishi wao na kipenzi chao, Dk. Tulia Ackson akitua kwa helikopta ya kijeshi.

Naam, ni Dk Tulia, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano aliyekuwa akitua nyumbani Mbeya, baada ya kuandika historia na kuitangaza vizuri Tanzania kimataifa kwa kushinda kiti cha Urais wa Mabunge Duniani (IPU).

Siku hiyo ilikuwa ya aina yake kwani badala ya helikopta iliyokuwa imembeba kiongozi huyo kutua kwenye Kiwanja cha Ndege cha Songwe, ilitua katika Uwanja wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) jijini Mbeya.

Veta ipo juu ya vilima vilivyopo karibu na Uwanja wa Ruanda Nzovwe ambao ulifurika wakazi wa mkoa huo na wengine wakitoa mikoa jirani kuja kumpokea shujaa Tulia anayetabiriwa makubwa katika uongozi wa nchi yetu.

Bila kujali tishio la mvua zinazoendelea kunyesha nchini kote, wakazi wa Mbeya walifurika kwenye uwanja huo kwa ajili ya mapokezi hayo maalumu yaliyoongozwa na ofisi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa huo, kwa lengo la kumpongeza Dk Tulia kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa IPU.

Katibu wa Siasa na Uenezi CCM mkoa wa Mbeya, Christopher Uhagile anasema mapokezi yameshirikisha wakazi mbalimbali wa mkoa wa Mbeya pamoja na mikoa jirani na kwamba ni ishara ya kumshukuru Rais Dk Samia Suluhu Hassan kwani ana mchango wake katika kumwezesha Dk Tulia kupata wadhifa mpya.

Uhagile pia anaishukuru dunia kwa kumchagua Dk Tulia kuwa rais wa IPU, akiwa ni mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo.

Mwingine aliyeshiriki katika mapokezi hayo ni Mjumbe was Halmashauri Kuu ya CCM taifa mkoani Mbeya, Ndele Mwaselela. Mwaselela katika kauli yake anamkaribisha rais huyo mpya wa mabunge duniani na kumhakikishia kwamba yupo salama ndani ya CCM na Mbeya kwa ujumla.

Viongozi wengine waliokuwapo ni machifu, viongozi wa dini na Mkuu wa mkoa huo, Juma Homera.

Pamoja na kupigwa butwaa kwa wingi wa watu waliohudhuria mapokezi hayo, Dk Tulia anasema sifa zote ziende kwa Dk Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani ndiye ufunguo wa mafanikio yake katika IPU.

Anasema kuchaguliwa kwake pamoja na mambo mengine kumechangiwa na uongozi shupavu wa Rais Samia ambaye ameimarisha diplomasia ya kimataifa na kufanya watu wengi waizungumze Tanzania vizuri.

Anasema Rais Samia pia ameuheshimisha mkoa wa Mbeya kwani ndiye amechangia mambo mengi katika ushindi wake na kwamba ushindi huo ni zawadi kwa Tanzania nzima na Mkoa wa Mbeya kwa ujumla.

"Mheshimiwa Rais anazidi kuujenga upya mkoa wa Mbeya kwani ameleta miradi mingi katika kila wilaya... Lakini kwa Jiji la Mbeya, wananchi wanatambua wazi kwamba kwa kipindi cha miaka 10 ya wapinzani, jiji lilikuwa 'likizo' kimaendeleo," anasema.

Dk Tulia anawaambia wakazi wa Mbeya kwamba kutokana na nia nzuri ya Rais Dk Samia katika kusambaza maendeleo nchi nzima ikiwemo Mbeya, wanashuhudia ujenzi wa barabara ya njia nne kuanzia Nsalaga hadi Ifisi.

"Pia wakazi wa Mbeya watashuhudia ujenzi wa barabara ya mchepuko kutoka Mlima Nyoka kupitia Uyole ya Zamani – Mwansanga hadi Magereza Songwe," anasema.

Anasema kutokana na wakazi wa Mbeya kuiamini Serikali yake, Rais Samia ameamua kuwaletea maji ya uhakika kutoka Kiwira wilayani Rungwe hadi katika jiji la Mbeya.

Ni kwa muktadha huo, Dk Tulia anawasihi wakazi wa mkoa wa Mbeya kuendelea kuiamini Serikali ya CCM inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwani ana hakika Mbeya itazidi kung'ara.

"Nawaombeni wana-Mbeya msiwasikilize wanaosema hakuna kinachofanyika. Hawa ni wapinga maendeleo. Nyie endeleeni kumheshimu na kumuunga mkono Rais Samia ambaye ameamua kuwaheshimu wakazi wa Mkoa wa Mbeya," anasema.

Anawasihi wakazi wa Jiji la Mbeya kuwakataa wanaotaka kuvuruga amani ya mkoa na nchi kwa ujumla huku akisisitiza kwamba Mbeya ya sasa inatakiwa iwe kioo kwa utulivu.

Katika mapokezi hayo viongozi kadhaa walitoa kauli kuhusu ushindi wa Dk Tulia kwenye kinyang'anyiro cha urais wa IPU wakisema mbali na kulipa heshima kubwa Tanzania pia ameiheshimisha Mbeya.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya,

> **Mheshimiwa Rais anazidi kuujenga upya mkoa wa Mbeya kwani ameleta miradi mingi katika kila wilaya... Lakini kwa Jiji la Mbeya, wananchi...**

Juma Homera anasema utulivu wa mkoa wa Mbeya umechangiwa sana na uongozi wa Dk Tulia ambaye mara kadhaa amesuluhisha migogoro na changamoto mbalimbali.

Anasema utulivu wa Tulia na ushawishi wake umesababisha pia Serikali ya Rais Samaia kuleta fedha nyingi mkoani Mbeya katika sekta za afya, elimu, maji, barabara na kwamba heshima ya mkoa sasa imerudi baada ya miaka 10 kuwa chini ya upinzani bila kuwa na maendeleo ya maana.

Anauhakikishia umma wa wana-Mbeya kwamba mkoa wake, na hususani jiji la Mbeya halitakuwa tena kitovu cha vurugu bali ni mahali pa amani, mshikamano na watu kufanya biashara kwa utulivu.

Hata hivyo, anaweka wazi kwamba wanasiasa wanaotukana matusi badala ya kunadi sera za vyama vyao wataendelea kushughulikiwa kwani nchi ina utawala wa sheria.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Maji ambaye pia ni Mbunge wa Viti Maalumu mkoa wa Mbeya, Maryprisca Mahundi anasema wakazi wa Mbeya hawana budi kumshukuru sana Rais Samia kwa jinsi anavyoongoza nchi akipeleka miradi ya maendeleo kila mahala ukiwemo mkoa wa Mbeya.

Anasema Dk Samia hana roho mbaya wala roho ya kwa nini na kwamba ndiyo maana Mkoa wa Mbeya sasa unasonga mbele kimaendeleo baada ya kuona Dk Tulia ameutuliza mkoa.

Mbunge wa Jimbo la Makete mkoani Njombe, Festo Sanga akizungumza kwenye hafla hiyo anasema Dk Tulia ni kiongozi wa wabunge wote wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na kwamba kazi hiyo anaifanya vizuri.

Anakishauri Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuendelea kumpa heshma Dk Tulia akisema asiwepo wa kuchukua fomu 2025 ndani ya CCM kwa ajili ya ubunge wa Jiji la Mbeya.

Mbunge wa Jimbo la Mbarali mkoani Songwe, Bahati Ndingo anasema dunia itawashangaa wakazi wa Mbeya kama hawatamuunga mkono Dk Tulia katika masuala ya maendeleo ambayo yanafanywa kwa manufaa ya mkoa na nchi kwa ujumla.

Hafla hiyo ya mapokezi ya Dk Tulia ilipambwa na burudani kutoka vikundi mbalimbali vya utamaduni.



**Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Mabunge Duniani (IPU), Dk Tulia Ackson akiwasili Mbeya siku chache baada ya kushinda kiti hicho. Dk Tulia (mwenye miwani) ambaye pia ni Mbunge wa Jiji la Mbeya akisalimiana na Naibu Waziri wa Maji na Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi.**

Jarida hili haliuzwi

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

| Jumatano Novemba 15 - 21, 2023 |




# Hii kauli ya Lema ina ukakasi mkubwa



UK. 12 & 13

Afya



# Matumizi ya simu za mkononi huchangia kupunguza nguvu za kiume kwa vijana?

**Na Mwandishi wa BBC**

WATAFITI wamegundua uhusiano kati ya matumizi ya simu za mkononi na kupungua kwa idadi ya mbegu za kiume za uzazi kwa vijana.

Kiwango cha mbegu za kiume ulimwenguni, kimekuwa kikipungua kwa miongo kadhaa sasa na ijapokuwa watalaamu wana sababu nyingi wanazohisi zinachangia hali hiyo, hakuna anayefahamu hasa ni kwa nini hali iko hivyo.

Katika utafiti mpya kutoka Uswisi, huenda ukaongeza kwenye orodha hiyo sababu nyingine inayochangiwa na simu za mkononi.

Baada ya kuufanyia utafiti sampuli za mbegu za kiume za zaidi ya vijana 2,800, watafiti wa Uswisi walipata uhusiano kati ya matumizi ya juu ya simu za mkononi na kiwango cha chini cha mbegu za kiume. Utafiti huo ulichapishwa katika Jarida la Uzazi na Utasa.

Hawakupata tofauti katika uwezo wa kusafiri mbegu za kiume kwenye uke au muundo kati ya aina tofauti ya watumiaji wa simu.

Kadhalika, hawakupata ushahidi wowote unaoonyesha kuwa kuiweka simu mfukoni badala ya begi la mgongoni, kwa mfano, kunachangia katika ukolezi wa mbegu za kiume.

Watafiti hao walifanya uchunguzi huo kutoka mwaka wa 2005 hadi 2018 na kubaini kuwa uhusiano kati ya matumizi makubwa ya simu na kiwango cha chini cha mbegu za kiume, ulionekana wazi zaidi katika miaka ya mwanzo ya utafiti huo kuliko mwishoni.

"Muundo huo unatokana na mabadiliko ya teknolojia mji, hasa kutoka mitandao ya 2G hadi 3G na 4G na kupungua kwa nguvu za simu.

## BADO HAKUNA MAELEZO YA BIOLOJIA YALIYOFANYWA

Utafiti huu unaongeza simu za mkononi kwenye orodha ndefu ya sababu ambazo watafiti wengine waligundua kuwa huenda zikaharibu uzazi.

Mfano, kuvuta sigara, shinikizo la kisaikolojia, pombe, kunenepa kupita kiasi na kemikali zinazopatikana kwenye sumu za kuwaua wadudu na mifuko ya plastiki inayofungia mboga tunazonunua madukani.

Hata hivyo, Profesa Allan Pacy, wa afya ya wanaume kutoka Chuo Kikuu cha Manchester ambaye hakuhusika katika utafiti huo, anasema utafiti huo siyo kamilifu, na watayarishaji wa ripoti hiyo wanakiri hilo, lakini ni utafiti katika ulimwengu halisi na kwa maoni yake hicho ni kitu kizuri.

Alison Campbell, mwanasayansi Mkuu wa Care Fertility, ameuita utafiti huo kuwa "wa kufurahisha na ambao haujawahi kuonekana". Hakushiriki katika utafiti huo.

Lakini Campbell anasema huenda kukawa na maelezo mengine ya kupungua kwa idadi ya mbegu za kiume miongoni mwa watumiaji wa mara kwa mara wa simu za mkononi.

Pacey anaunga mkono wasiwasi huo. "Hatuwezi kuwa na uhakika kuwa simu ya mkononi siyo ishara mbadala kwa kipengele kingine cha mtindo wa wanaume au taaluma yao,"

Anaongeza kwamba hiyo ndiyo sababu halisi ya mabadiliko yoyote kwa ubora wa mbegu za kiume.

"Kwa sasa, hakuna maelezo yaliyothibitishwa ya biolojia au mifumo inayotokana na uchunguzi huu, kwa sababu utafiti bado haujafanyika," anasema.

## WANAUME WANAPASWA KUFANYA NINI?

Kama wewe ni mwanaume unayepanga kuwa na watoto katia maisha yako, habari hizi huenda zikakupa wasiwasi, lakini watafiti wanasema usiwe na hofu wala kufanya mabadiliko makubwa kwa sasa.

"Kama wanaume wana wasiwasi, basi kuweka simu zao mkobani na kupunguza matumizi ya simu, ni kitu rahisi cha wao kufanya," anasema Pacy.

Lakini kwa sasa hakuna ushahidi kuwa hiyo itaongeza ubora wa mbegu zao za kiume.

"Kwangu mimi, nitaendelea kuiweka simu yangu kwenye mfuko wangu wa suruali," anasema huku akiweka simu yake kwenye mfuko wa suruali.

Kolamu



Hamisi Kibari

## TUKUBALIANE KUTOKUBALIANA

Simu: 0758143457

# Mpira si uadui



INGAWA mimi si mchambuzi wa mpira wa miguu, lakini ninaufuatilia. Michezo mingine ninayopenda kuangalia ni riadha na mpira wa kikapu.

Nilipokuwa shule ya msingi, nilikuwa ninacheza mpira wa miguu hadi kuwa tegemeo kwenye timu ya darasa, lakini kabla sijachaguliwa kwenye timu ya shule, nikanogewa na mpira wa kikapu.

Pamoja na kucheza mpira wa kikapu, nimeendelea kuwa mpenzi wa mpira wa miguu kiasi kwamba huko nyuma ilikuwa ni nadra kukosa viwanjani ninapokuwa na nafasi.

Nakumbuka nilipokuwa mdogo pale Uwanja wa Karume, Mjini Musoma, nikikosa kiingilio, ninasubiri hadi ule wakati wa 'fungulia mbwa' angalau niburudike hata kwa zile dakika tano tu kama si chini ya hapo kabla ya mechi kwisha!

Kuna hii siku niliruka ukuta nikanusurika kung'atwa na jibwa la polisi likiwa linaongozwa na askari mmoja mbabe aliyejipatia sifa sana wakati huo, akijulikana kwa jina utani, Ching'ong'o. Nikakoma!

Kama walivyo Watanzania wengi, hata mimi nilijikuta nikiwa shabiki wa moja ya timu zetu mbili kubwa na kongwe hapa nchini, ushabiki ambao nimeshindwa kuuacha.

Ilikuwaje? Wakati nikisoma madrasa kwa Sheikh Othman Magee (Mungu amrehemu), siku za Jumapili ambapo wanafunzi tunakuwa wengi, wakati wa mapumziko saa nne mpaka saa tano, tulikuwa tunajigawa huku na kule, tunacheza mpira wa matambara.

Siku moja, mwanafunzi mwenzetu kiongozi ambaye alikuja kuchezea Yanga, Ally Juma Mchumila, alishauri tucheze Yanga na Simba. Wale ambao hatukuwa na upande wowote hadi wakati huo akatuchagulia upande wa kuchezea. Ajabu! Kuanzia siku hiyo nikawa shabiki wa upande wa timu aliyonichagulia!

Kwa kipindi kirefu, niliuona ushabiki wa Yanga na Simba kuwa utani tu wa jadi kama inavyonenwa. Kwamba timu hizi zinapochuana, au moja kuchukua ubingwa, anayeshinda anamtambia aliyeshindwa, maisha yanaendelea.

Nyumbani kwetu, tumegawanyika pia. Wapo wapenzi wa Yanga na wengine ni Simba, lakini hatujawahi kuhasimiana zaidi ya kutambiana. Nimeziona pia familia nyingi ambazo baba ni Simba na mama ni Yanga au kinyume chake, lakini wanaishia kutambiana na kufanyia masihara, basi.

Ninakumbuka miaka ya 1990, baada ya timu zetu za ndani kutofanya vizuri kwa muda mrefu, siku moja Simba ilikuwa inacheza na timu kutoka nje ya nchi, wapenzi wa Yanga wakaishangalia Simba.

Lakini ikaja siku nyingine ambayo wapenzi wa moja timu hizi, waliamua kutoipa nguvu ya kushangilia timu ya nyumbani ikicheza na ya nje, wakidai 'uzalendo umewashinda'. Neno hili lilianzia kwenye soka kabla kutumika kwingineko.

Hata hivyo, kwa mtazamo wangu katika miaka ya karibuni, ushabiki wa Yanga na Simba unageuka taratibu kuwa mithili ya uhasama, uadui ama katika maeneo mengine vita kabisa!

Niliwahi kuona klipu moja pale Morogoro, mashabiki wa Yanga wakimtimua kwenye jukwaa 'lao' shabiki wa Simba kisharishari. Juzi kati nikaona klipu nyingine, ikionesha mashabiki wa Simba wakimsulubu shabiki wa Yanga katika hali iliyokuwa inatishia uhai wake.

Nimeona taarifa ya Simba wakionesha kusikitishwa na kitendo hicho. Ni hatua ya kupongeza, lakini makemeo na hatua zinazochukuliwa na wadau, TFF na hata serikali kulaani tukio halo, kama lilivyokuwa lile la Morogoro si za kuridhisha sana.

Kama Bodi ya Ligi huwa inachukua hatua dhidi ya kocha kuingia uwanjani amevaa kaptura au mashabiki kurusha chupa, ninatazamia katika hili bodi hiyo ichukue hatua kali zaidi kwa sababu hapa tunazungumzia uhai wa mtu.

Baada ya Simba kufungwa na Yanga magoli 1-5 Novemba 5, pia nimeona mambo yanayopindukia utani wa kawaida. Nimeona picha ya mwanamke, shabiki wa Yanga akiwa amepigwa na mumewe ambaye ni shabiki wa Simba nusura ya kumtoa jicho. Baada ya mechi, niliona mtu uwanjani akizuiwa kujirusha ili kujitoa uhai na wengine wakidai hawawezi kurudi makwao baada ya kipigo!

Hata kwenye makundi sogozi, nimeona pia watu wakirushiana maneno makali hadi wengine kuamua 'kulefti'.

Nimeandika makala haya kufuatia picha mbili muhimu sana zinazotukumbusha kwamba mpira na michezo mingine, si uadui. Moja ilikuwa picha ya mchezaji wa Simba, Jean Baleke akiwa na wachezaji wa Yanga baada ya kumalizika kwa mechi ambayo Simba ilifungwa.

Kuna wapenzi wa Simba ni kama wanamshangaa pengine wakitaka sijui alie, lakini alichoonesha Baleke ni kwamba mpira si uadui. Ningeshauri hata TFF wampongeze rasmi kwa hilo.

Lakini tukio lililonikuna zaidi ni la wasemaji wa vilabu hivi vikongwe, Ahmed Ally ana Ally Kamwe kuonekana wakiwa pamoja bungeni sambamba na Msemaji wa Yanga aliyefungiwa, Haji Manara.

Ni hatua nzuri inayosaidia kuonesha Watanzania kwamba mpira si uadui, wala hatuna sababu ya kununiana au kukerana hadi mtu kuogopa kurudi mtaani kwake kwa sababu ya mpira!

Binafsi, ninaamini hawa wasemaji wa vilabu hivi, wana mchango katika kutubakiza au kutuondoa kwenye hii hali ya kuhasimiana. Ninaamini pia wana mchango katika kutufikisha hapa, wakubali wakatae.

Labda nimzungumzie kidogo Haji Manara kadiri jicho langu linavyomwona. Ana historia nzuri kichwani mwake kuhusu mpira wetu. Ni mhamisishaji mzuri wa timu yake na amesaidia sana kuupa thamani mpira wetu.

Baada ya Simba kufungwa 1-5, inaoneka viongozi hadi wapenzi wa timu hiyo, wamevurugwa sana. Ninaamini kama Haji angekuwa bado yuko Simba, alikuwa ana uwezo wa kutuliza hali ya hewa.

Pengine Simba wasingefikia hatua ya kufukazana ambayo mimi naamini ililenga zaidi kuwatuliza mashabiki kwa sababu siamini Simba waliajiri kocha kwa ajili ya kuifunga Yanga tu. Kwamba kocha aliyeiingiza Simba makundi na kuitoa ulimi nje klabu bora Afrika, Al Ahly, anaweza kuonekana si chochote si lolote kwa mechi moja tu ya mtani wa jadi!

Hata hivyo, Haji ana mapungufu yake pia. Ana kauli zinazoamsha hasira na chuki upande mwingine wa shilingi.

Akiwa Msemaji wa Simba, kuna baadhi ya kauli alikuwa anazitoa kama utani, lakini zimetumiwa sana na watu kuhasimiana. Miongoni mwa hizo ni pale aliposema kwamba linapokuja suala la Yanga, wapenzi wote wa timu hiyo hukosa akili kasoro baba yake na Rais Mstaafu, Jakaya Kikwete. Ziko kauli nyingi, lakini ngoja nisiende huko.

Lakini juzi, kwa bahati mbaya sana, ametetea jambo ambalo si la kimichezo abadani. Labda nianze kuuliza swali hili. Katika matendo ya kiungwana au ya kihuni, kuzomea unaliweka fungu gani? Uungwana au uhuni?

Kuzomea ni kitendo cha kumvua thamani mwanadamu mwenzako na bila shaka hakuna yeyote anayependa kuzomewa. Hata Haji akiingia mahala akazomewa na wapenzi wa timu aliyokuwa akiisemea zamani, ni dhahiri kama binadamu hatajisikia vizuri. Vitabu vya dini vinasema, jambo usilotaka kufanyiwa, basi usiwafanyie wengine.

Nimeshangaa kusoma akitetea watu kumzomea Feisal Salum 'Fei Toto' kwa madai kwamba moja ya kazi ya mashabiki ni kuzomea! Hapana. Huwezi kutetea na kubariki kitendo cha kihuni. Huu si uanamichezo.

Kimsingi ninachosema hapa ni kwamba ni muhimu wasemaji wa vilabu vyetu vikubwa, wajitenge na maneno yanayoweza kuhamasisha uhasama. Pia waache kuwaaminisha wapenzi wao kwamba sasa timu zao ni zaidi ya Ahly au Barcelona.

Kuaminishwa huku ndiko kumekuwa kukiwafanya baadhi ya wapenzi wa timu hizi kutamba mitaani, wengine utadhani wana ushirikiano na Mungu kuropoka maneno kama vile: "Mtani akitufunga nitatembea uchi wa mnyama kutoka ponti A mpaka B" au "Niko tayari kuvaa dera tukifungwa". Hivi mtu anayetoa ahadi za ajabu kama hizi, timu yake ikifungwa atarejea vipi mtaani kwake?

Mtu yeyote akiweka kando ushabiki, hataacha kukiri kwamba Yanga iko vizuri kwa sasa kulinganisha na watani wao na hivyo Simba kufungwa goli tano, si ajabu ingawa katika dabi (derby), Yanga ingeweza kufungwa pia.

Uhasama wa Simba na Yanga, umekwenda mpaka kwenye timu ya Taifa. Stars inapofanya vibaya watu wanazodoa wachezaji kutokana na timu zao. Tutaimarishaje na kuishangilia Stars kama tumegawanyika kwa kuangilia u-Simba na u-Yanga?

Ni vyema tuturudi kwenye mstari. Mpira si uhasama bali ni burudani. Kwa nini ukuumize utadhani umefiwa? Brazii ilifungwa goli saba na Ujerumani mbele ya wapenzi wao, mbona walichukulia poa tu?

Siasa

# Hii kauli ya Lema ina ukakasi



**Na Hamid Yassin**

MJUMBE wa Baraza Kuu la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Godbless Lema anasakwa na vyombo vya dola kwa tuhuma za kumtishia maisha Mtendaji wa Kijiji cha Korongwe, Daud Ismail wilayani Nkasi, Mkoa wa Rukwa.

Agizo la kukamatwa kwa Lema lilitolewa hivi karibuni na Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijualikali. Kiongozi huyo ametaka Lema ahojiwe kwa kutoa kauli za uchochezi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika Oktoba 24, 2023 katika kijiji hicho kilichopo kitongoji vya Forodhani, Kata ya Fipa.

Mpaka ninaandika makala haya, hakukuwa na taarifa za Lema kukamatwa, lakini alikaririwa akisema yuko 'Kijiweni' Arusha na kwamba anayemtaka akamkamate.'

Kiongozi huyo ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Chadema Kanda ya Kaskazini, anaonekana katika video ambayo inasambaa kwenye mitandao ya kijamii, akihamasisha wanaume wa Kijiji cha Korongwe Asilia, 'wamuue' mtendaji wa kijiji chao kwa madai ya kuwasumbua wananchi.

Kwenye video hiyo, Lema akiwa na baadhi ya viongozi, wanachama na wafuasi wa Chadema katika eneo hilo la Korongwe, anaonekana akitamka neno ambalo limetafsiriwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Lijualikali kuwa, ni kutaka wanaume wamuue mtendaji anayewasumbua.

# Siasa


Lijualikali



Lijualikali amesema kuwa, haiwezekani kiongozi mwenye ushawishi mkubwa wa watu aachiwe kutamba kwa kauli hiyo ambayo imesababisha taharuki kwa wananchi na mtendaji huyo ambaye kwa sasa maisha yake yako shakani, huku kiwango cha utendaji kikishuka kijijini hapo.

"Namuagiza OCD (Kamanda wa polisi wa wilaya) wa Nkasi, kuchukua hatua za kisheria mara moja kumwita kokote aliko Godbless Lema ili afike Nkasi afanyiwe mahojiano kuhusu kauli yake ya kichochezi na ya kuhatarisha hali ya usalama ya mtendaji huyo katika eneo letu. Kauli hiyo pia inakwaza juhudi za wananchi kufanya shughuli za maendeleo," amekaririwa Lijualikali akisema.

Akijibu swali ni kwa nini jambo hilo lilitokea muda mrefu lakini wamechelewa kutoa taarifa, Mkuu wa Wilaya amesema walianza kwa kufanya uchunguzi kuhusu kauli hiyo kujua ina maana gani na ililenga nini kitokee. Amesema wamejiridhisha kwamba haikuwa kauli nzuri.

"Badala ya kutumia nafasi ya kujinadi na kujitangaza, wameigeuza fursa waliyopewa na Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuwa jukwaa la kutukana mamlaka. Wanatukana viongozi wa nchi. Ukiwasikiliza vizuri, utaona wanatusi, wanakebehi, kubeza na kuwatweza Watanzania na nchi yetu kwa ujumla," amefafanua Lijualikali.

Alipoulizwa kuhusu kauli hiyo, Lema amekiri kuwepo katika mkutano huo na kueleza alichotamka ni kuwataka wananchi 'wamuoe' mtendaji anayewasumbua siyo 'wamuue' na kusisitiza kuwa hawezi kutamka hivyo.

"Hizo ni lugha za kisiasa, waambie wasikilize hiyo klipu vizuri. Siwezi kutoa kauli kama hiyo kwa kiongozi. Nilichotamka pale ni kuwaambia kama mtendaji anawasumbua basi muoeni, lakini suala la kuua halikuwa sehemu ya hotuba yangu," amedai Lema.

Mtendaji huyo, Daud Ismail amekiri kusikia taarifa ya vitisho kutoka kwa Lema ambayo anasema amesababisha maisha yake kuwa mashakani na utendaji kazi wake sasa umekuwa wa hofu, ikizingatiwa kwamba wanafanya kazi mipakani, kwenye eneo lenye matukio mengi.

Daudi amesema kiongozi kama Lema anapotoa kauli tata kwa maisha ya mtu mdogo kama yeye (mtendaji) inatia shaka kwa kuwa anasikilizwa na wafuasi wengi wa chama chake na hata vyama vingine hivyo huwezi kujua ndani yake kuna nini.

Hebu sasa tuijadili kwa kina kidogo kauli hii ya Lema, iwe ni kuua au kuoa, ni sahihi kutamkwa na kiongozi kama yeye?

Kiongozi huyu mwandamizi wa Chadema anasema hakutamka mtendaji huyo auawe, bali anakiri kabisa kwamba "aliwataka wanaume wa kijiji hicho wamuoe"!

Yaani wanaume wamuoe mwanaume mwenzao, siyo? Hivi kiongozi makini ambaye kila siku anapigania chama chake kishike dola ya kuongoza nchi anaweza kuongea lugha ya kutaka wanaume wamuoe mwanaume mwenzao mbele ya hadhira ya watu?

Hapa Lema atasema anaipigania Chadema ama anaihujumu? Wananchi gani wenye akili timamu wanaweza kumuunga mkono yeye mwenyewe ama chama chake kwa kauli kama hii ya kihuni kama si uendawazimu?

Umefika wakati viongozi hawa wa kisiasa wawe wanapimwa akili zao ijulikane iwapo wako timilifu vichwani mwao ama la, kama ilivyowahi kupendekezwa kule bungeni miaka michache iliyopita!

Kwa wanaotunza kumbukumbu, hii si mara ya kwanza kwa Lema kutoa kauli tata na za udhalilishaji kwa viongozi na watendaji mbalimbali wa taifa hili.

Wakati fulani akiwa Mbunge wa Arusha Mjini, Lema aliwahi kutoa kauli ambazo hata mtoto wa darasa la kwanza hawezi kuongea akiwa ndani ya chombo kikubwa cha kutunga sheria, yaani ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini yeye alifanya hivyo!

Kwa wale wanaokumbuka kwani klipu za alichokisema zilizosambaa mitandaoni, mwanasiasa huyo alionekana akimtabiria kifo aliyekuwa kiongozi mmoja mkubwa wa taifa hili! Kwamba angefariki dunia kabla ya mwaka 2020!

'Utabiri' alioutoa Lema Bungeni ndiyo ulikuwa mwanzo wa baadhi ya wabunge kutaka kuwe na utaratibu wa kuwapima akili viongozi na wawakilishi wa watu hususani kung'amua wale wanaotumia bangi na dawa nyingine za kulevya.

Mimi niliwaunga mkono kwa asilimia mia wabunge wale, kwani kwa kauli ile ya Lema ni ukweli usiopingika kuwa maneno yale aliyasema akiwa hayuko sawa kichwani!

Vitu vya kujiuliza hapa Watanzania wenzangu na kutafakari kwa kina hivi hii jeuri ya kutoa kauli tata mara kwa mara Lema anaitoa wapi? Kitu gani huwa kinamsukuma mpaka kujiamini mpaka kutoa matamko kama hayo?

Je, kuna watu nyuma yake wanaomlinda? Kama wapo ni akina nani hao? Maana katika hili sakata la kule Korongwe Nkasi, Lema amejibu kwa jeuri kwamba yuko kijiweni Arusha anasubiri hivyo vyombo vya dola vikamkamate!

Huyu karudi nchini Machi mwaka huu baada ya kukimbia nchi tangu mwaka 2020 kwa sababu ambazo ninaweza kusema alijitungia tu. Hivi hii haiwezekani kwamba anaweka mtego kwa Serikali wamswekwe 'lupango' ili ionekane Tanzania haina utawala wa kisheria?

Huyu alihifadhiwa Canada kwa miaka karibu miwili. Moja ya vitu ambavyo inaelezwa kwamba vimekuwa vikisaidia Chadema kufadhiliwa na wazungu huko nje ni uongo.

Kwa kuwa wanakula fedha zao na kupokea misaada yao mbalimbali au kukimbia huko kujificha, bila shaka wamekuwa wakitaka kuwaonesha kwamba wanapambania demokrasia Tanzania lakini wanakwazwa na mamlaka, kumbe ni maigizo matupu na uvunjifu wa sheria za nchi!

Ninamaanisha kwamba wamekuwa na kawaida ya kuanzisha tafrani na vyombo vya dola na wanapodhibitiwa na vyombo hivyo hurekodi matukio hayo na kutuma klipu huko kwa wahisani wao kuonesha kwamba licha kupambana kutaka kushika kwa njia ya demokrasia lakini wanahujumiwa na serikali iliyoko madarakani!

Udhalilishaji huu uliofanywa na Lema dhidi ya Mtendaji Daudi ungefanywa na viongozi wa Serikali ama CCM, bila shaka sasa hivi ungesikia kelele nyingi ndani na nje ya nchi.

Wako wapi wale wanaojiita watetezi wa haki za binadamu? Lema amekiri kwamba amewataka wanaume wa kijiji cha Korongwe wamuoe mtendaji wao, mwanaume mwenzao Daudi Ismail. Haya si ndio mapenzi ya jinsia moja ambayo hapa kwetu Tanzania hayakubaliki!

Kauli hii ingekuwa imetamkwa na kiongozi wa chama tawala dhidi ya wale wa upinzani, hizi taasisi za haki za binadamu zingekaa kimya? Je, viongozi wa vyama vya upinzani wangekaa kimya na kuona ni jambo la kawaida kama ilivyo sasa?

Wanakijiji wamuoe vipi mwanaume mwenzao mwenye familia yake na kiongozi wao aliyewekwa pale kihalali? Maana yake nini? Yaani anataka wambake kinyume na maumbile siyo? Hivi agizo lake likitekelezwa si ndio mauaji yenyewe haya anayozungumzia Mkuu wa Wilaya ya Nkasi?

Tunaelewa kwamba Chadema kupitia Makamu Mwenyekiti wao, Tundu Lissu amekuwa mtetezi wa mapenzi ya jinsia moja, jambo linalotokana na masharti ya kuendelea kupatiwa misaada na wafadhili wao wa kule ughaibuni.

Hapa kwetu Tanzania kuanzia Serikali ya Awamu ya Kwanza hadi hii ya sita jambo hili la mapenzi ya jinsia moja ni marufuku! Inakuaje Lema anahamasisha watu wamuoe kiongozi mwanaume kama madai yake ni sahihi? Hata angekuwa mwanamke, kubakwa na wanakijiji ni uuaji na adhabu yake si chini ya miaka thelathini jela!

Mwisho nashauri vyombo vyetu vya ulinzi na usalama visiwe vinapuuza kauli kama hizi. Waswahili wanasema lisemwalo lipo na kama halipo laja, fanyeni uchunguzi wa kina dhidi ya kauli hii tata ya Lema.

Viongozi wote wa taifa hili kuanzia wale wa serikali, taasisi za umma na binafsi, na hata vyama vya upinzani wanatakiwa kuunga mkono na kutekeleza sera za Chama tawala, kwani ndicho kinachoshika hatamu kwa sasa!

Jamii

# Tuwe na kampeni ya ‘Kawia Ufike, Jali Maisha’

**Na Reubeni Lumbagala, Kongwa**

NI dhahiri shahiri, ajali za barabarani zimeongezeka.

Kinachokera zaidi ni ukweli kwamba asilimia kubwa ya ajali hizi inatokana na uzembe, yaani mambo kama kuendesha ilihali dereva kalewa na kutofuata sheria za barabarani kama kuendesha kwa kasi kubwa, kuyapita magari (overtaking) bila kuzingatia sheria, kuendesha gari likiwa na kasoro mbalimbali na kadhalika na kadhalika.

Kutokana na hali hii, hatua thabiti zinapaswa kuchukuliwa na kila mdau ili kukomesha au kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali hizo ambazo kimsingi zimekuwa zikikatisha uhai wa watu, kusababisha ulemavu wa kudumu, ongezeko la yatima, wajane na wagane.

Vilevile ajali zimekuwa zikisababisha kuwepo kwa matumizi ya fedha katika kusafirisha na kuuguza majeruhi, fedha ambazo yamkini zingeweza kutumika katika matumizi mengine ya maendeleo endapo ajali hizo zisingetokea.

Ajali pia zinamaliza raslimali muda kwani majeruhi wa ajali mara nyingi hukaa mahospitalini au majumbani wakiuguza majeraha kwa siku kama si miezi kadhaa, muda ambao ungetumika kwa ajili ya kuzalisha.

Agosti 30, 2023, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Camilius Wambura akiwa Moshi mkoani Kilimanjaro wakati wa kikao kazi cha maafisa waandamizi wa Jeshi la Polisi makao makuu, makamanda wa polisi wa mikoa na vikosi, alisema ajali za barabarani zimeongezeka kutoka ajali 858 Juni, 2021 hadi kufikia ajali 955 Juni, 2022, ikiwa ni ongezeko la ajali 97, sawa na asilimia 11.3.

IGP Wambura anakiri pia kwamba kupitia tathmini waliyoifanya, ongezeko hili la ajali limetokana na mwendo kasi na uzembe wa madereva wa vyombo vya moto, yaani magari pamoja na bodaboda.

Kutokana na ongezeko la ajali za barabarani, madereva na watumiaji wengine wa barabara wanapaswa kuwa makini wawapo barabarani ili kuepuka ajali ambazo zinazuilika.

Nasema hivyo kwa sababu yapo mazingira ambayo abiria hawapaswi kumvumilia au kumwonea haya dereva anayeonekana amelewa au anakiuka sheria za barabarani ikiwemo mwendokasi.

Hii si tu kwenye usafiri wa umma kama basi au daladala, bali hata gari la kampuni na gari binafsi. Ukikaa tu pembeni au nyuma ya dereva, jipe kibarua cha kuangalia namna anavyoendesha.

Halikadhalika ukipanda bodaboda, anza kwa kumweleza kwamba hautaki mwendo kasi na unataka afuate sheria za barabarani muda wote wa safari yenu. Na kwa kuwa kwenye bodaboda tunalipa baada ya kufika mwisho wa safari, asipotii masharti yako, mwambie asimamishe pikipiki, shuka na uchukue nyingine.

Elimu kwa umma ni muhimu kuendelea kutolewa kwa wananchi wote ili kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani. Binafsi, napendekeza Jeshi la Polisi kupitia kitengo cha Usalama Barabarani kuja na kampeni yenye kaulimbiu: “Kawia Ufike, Jali Maisha”.

Mwendokasi umekuwa sababu kubwa ya ajali nyingi za barabarani. Baadhi ya madereva wa vyombo vya moto wamekuwa na haraka ya kufika wanapokwenda, na hivyo kuendesha kwa mwendo ambao mwisho wake, unagharimu maisha yao, abiria na watumiaji wengine wa barabara. Wahenga walisema “Haraka haraka haina baraka”. Methali hii inasisitiza juu ya kuepuka kufanya jambo kwa haraka kwani mwisho wake unaweza usiwe mzuri.

Kampeni ya “Kawia Ufike, Jali Maisha” iweke mkazo kwa madereva kuendesha vyombo vya moto kwa mwendo wa wastani ambao hata kukitokea ajali kwa bahati mbaya, athari zake huwa ni ndogo, tofauti na ajali inapotokea wakati chombo kikiwa katika mwendokasi.

Kampeni isisitize kuwa ni bora kukawia kufika lakini ufike salama, kuliko papara za kutaka kufika haraka kwa kuendesha mwendokasi ambao ni chanzo kikubwa cha ajali.

Lengo la wasafiri ni kufika salama kule waendapo bila kutokea matatizo njiani. Kampeni itilie mkazo uendeshaji wa vyombo vya moto kwa mwendo wa wastani ambao utasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani.

Endapo madereva wa vyombo vya moto; magari na pikipiki, watazingatia kikamilifu umuhimu wa kufika salama, watachukua tahadhari kubwa katika uendeshaji wao kwa kuzingatia alama za barabarani.

Katika kampeni hii, tunaweza pia kuiga nchi moja ambayo mabango ya kuwataka madereva kuendesha mwendo ambao si hatarishi yaliwekwa katika kila maeneo ambapo madareva na abiria wana kawaida ya kwenda kujisaidia na kula chakula.

Kwa mfano, kwa wasafiri wa Dar es Salaam hadi Mwanza au Dar Arsusha, kuna mahoteli ambako husimama wao na madereva kwa ajili ya kujisaidia na kula. Katika mahoteli hayo mabango yanapaswa kubandikwa kuanzia vyooni wanamoingia kujisaidia, kwenye maeneo ya kulia chakula hadi maeneo ya kuegesha magari.

Uhai wa watu ni jambo lenye thamani kubwa ambao kamwe haliwezi kulinganishwa na chochote. Madereva wanapaswa kujali maisha yao, ya abiria na watumiaji wengine wa barabara kama vile watembea kwa miguu na wasukuma mikokoteni.

Njia mojawapo ya madereva kujali maisha yao ni kuepuka kuendesha vyombo vya moto kwa mwendokasi na kuzingatia sheria na alama za barabarani.

Madereva hawapaswi kuwa sababu ya abiria kujuta kupanda vyombo vyao vya moto kwa kuendesha kwa mwendokasi ambao unahatarisha maisha ya watu.

Wamiliki wa vyombo vya moto na hapa ninakusidia zaidi vyombo kama mabasi na bodaboda, pia wana mchango wao katika hili. Ni muhimu wahakikishe wanaajiri madereva wenye lesani, wenye tabia nzuri na ambao takwimu zinaonesha wanaendesha magari au pikiliki kwa weledi na uadilifu.

Hata baada ya kuwaajiri, wanapaswa kuendelea kuwafuatilia kama madereva wao wanazingatia ipasavyo sheria za usalama barabarani.

Hivi inakuwaje wewe mmiliki wa gari uajiri dereva mlevi au anaendesha gari kwa mwendo wa kasi. Licha ya kuweza kusababisha ajali, huoni kwamba anaweza pia kugongesha chombo chako na kikaharabika vibaya?

Kwa ushirikiano wa pamoja baina ya serikali, wamiliki wa vyombo vya moto, madereva, abiria na watumiaji wengine wa barabara, ajali za barabarani zinaweza kupungua kwa kiasi kikubwa. Yatosha sasa habari hizi za ajali za barabarani kila mara – Kawia Ufike, Jali Maisha.

*Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilayani Kongwa mkoani Dodoma. Mawasiliano yake ni: 0620-800462.*





# Maisha, maajabu na uwezo wa nungunungu

**Na Godfrey Sanga kwa Msaada wa Mitandao**

NUNGUNUNGU au nungu, ni wanyama wagugunaji wenye ngozi iliyotawaliwa na miiba iliyochongoka wanayoitumia kama moja ya kinga dhidi ya maadui.

Walitajwa kuoneakana kwa wingi na rahisi miaka mingi iliyopita.

Pia wanashika nafasi ya tatu katika wanyama wagugunaji kwa ukubwa, wakitanguliwa na capybara na buku.

Nungu wana urefu kati ya sentimita 20 na 25. Uzito wao ni kati ya kilo 5.4 na 16.

Wana umbo la duara, wakubwa na wataratibu. Nungunungu huwa katika rangi mbalimbali ya kijivu na mara chache nyeupe.

Hujihami kwa miiba pia hukaribiana kufanana na kule kwa kalunguyeye (Erinaceomorpha) na ekidna (Monotremata).

## SPISHI

Nungu ni miongoni mwa spishi 29 za wanyama wagugunaji (rodent) wa familia ya Erethizontidae au Hystricidae. Nungu wanatofautiana kwa ukubwa.

Nungu aitwaye Rothschild's Porcupine wa Amerika ya Kusini ana uzito pungufu ya kilo moja ukifananisha na wa Afrika.

Anaweza kukua mpaka kufikia kilo 10. Familia mbili hizi za nungu ni tofauti kabisa ingawa wote wapo kwenye tawi la Hystricognathi wa oda ya Rodentia, hawahusiani sana. Inaaminika kuwa wametokana na hystricognaths wengine takribani miaka milioni 30 iliyopita.

Nungu wa miaka ya leo, wana umbo dogo kwa kawaida huku miiba yao ikiwa imejishikiza mmoja mmoja badala ya makundi, pia hutajwa kuwa wakweaji wazuri, na hutumia muda wao mwingi juu ya miti.

## UMRI

Nungu kwa wastani wana uwezo wa kuishi muda mrefu na wanashikilia rekodi miongoni mwa familia yao ya rodent kwa kuishi kwa kiasi cha muda mrefu zaidi ambayo imevunjwa hivi karibuni na panya aina ya Naked Mole Rat (Heterocephalus glaber).

## MIIBA

Miiba ya nungu huchukua sura mbalimbali kulingana na spishi, lakini yote ni nywele zilizoboreshwa na kufunikwa na keratini, na zimejishikiza kwenye misuli ya ngozi.

Nungu wa kale (Hystricidae), wana miiba iliyojikusanya kwenye makundi huku kwa nungu wa miaka leo (Erethizontidae), miiba mmoja mmoja, imechanganyika na ufumwele yaani manyoya ya chini na nywele.

Miiba huachiwa kwa kuigusa au hudondoka pale ambapo nungu anajitikisa, lakini hawezi kamwe kurushwa kwa adui, pamoja na imani iliyozoeleka.

Miiba mipya hukua huchukua nafasi ya ile iliyopotea.

Mwiba huanza kuwa mwembamba na kujipinda unapokaribia kushikana na ngozi. Ndiyo sababu nungunungu hawezi kuchomwa na miiba yake hata akianguka kutoka mahali palipoinuka.

## MAKAZI

Nungu hupatikana sana katika maeneo ya kawaida na tropiki ya Italia, Afrika na Amerika ya Kusini na Kaskazini.

Nungu huishi kwenye misitu, jangwani sehemu zenye miamba, vilima na nyikani. Baadhi ya nungu wa miaka ya leo huishi kwenye miti, lakini nungu wa miaka milioni zaidi iliyopita, waliependelea zaidi ardhini.

Nungu hupatikana hata kwenye miamba katika ardhi yenye urefu wa mita hata zaidi ya 3,700. Nungu ni wanyama wanaopenda kuonekana au kujitokeza usiku zaidi.

Majira ya baridi kali, nungu hutumia muda mwingi akiwa amelala, ana tezi maalum inayomsaidia kusawazisha joto la mwili wake, majira haya hula kwa nadra sana hivyo hutumia mafuta ya ziada anayohifadhi mwilini mwake.

Ukijaribu kumfuga nungunungu, hupanda ukutani au kwenye bomba la maji na kuponyoka kwani anapenda kuishi katika eneo kubwa.

Na hii, diyo sababu, si rahisi kumfuga au kumfanya awe mnyama kipenzi, Ni vizuri zaidi kwamba hafugwi kwa kuwa yeye hubeba viroboto wengi sana siku zote.

## ULAJI

Nungu hupendelea zaidi chumvi, anapotafuta chumvi wakati mwingine wanaweza kufika mpaka makazi ya watu na hupendelea kukaa kwenye mbao zilizopakwa sodium naitreti, rangi za kuta, mishikio ya vifaa, viatu, nguo na vitu vingine vilivyopata jasho.

Nungu pia huvutiwa na barabara ambazo chumvi hutumika kuyeyusha barafu, na mara kadhaa huonekana wakilambalamba magurudumu ya gari zilizopita kwenye barabara hizo. Hutumia chumvi maalumu kama moja ya kuwaongezea kinga pindi wanapoumia kupona haraka.

Vyanzo vya asili vya chumvi ambavyo nungu hutumia hujumuisha mimea yenye chumvi chumvi, mifupa ya wanyama, magamba ya miti, matope kwenye udongo wenye chumvi sana, na vitu vilivyoshikwa na mkojo.

## IMANI POTOFU

Kwa kipindi kirefu, nungu huaminika kuwa na uwezo wa kurusha miiba yao kwa adui, hii imekanushwa vikali, baada ya kufahamu kuwa miiba hulegea na kuanguka yenyewe basi imepunguza hisia za watu kuhusisha na ushirikina. Kwani wengi wao waliamini endapo watakutana na mnyama huyu ni miiba kuanguka, basi kuna hatari ya kifo katika familia yao.

## USILOLIJUA

Ni vigumu sana kumuona kwa vile anaishi kwa shaka sana, kwani aonekanapo hushambuliwa na kuuawa kwa ajili ya kutengenezea dawa na kitoweo, wakati mwingine hukamatwa na kufugwa.

Anaposhtuliwa, nungunungu hujikinga kwa kujikunja kama mpira, Misuli yake yenye nguvu hukaza ngozi yake yenye miiba na kuufunika mwili mzima, Ngozi hiyo yenye miiba hufunika kichwa, mkia, miguu na sehemu zake za chini na anaweza kujikunja hivyo kwa muda mrefu.

Nungunungu huhisi njaa wakati wa jioni. Chakula chake cha jioni huwa wadudu na minyoo, lakini wakati mwingine anaweza kula panya, chura, mjusi au hata njugu na baadhi ya matunda.

Makala

# Umaskini na maendeleo Tanzania, vigezo gani vinatumika katika upimaji wake?

**Na Dk. Felician B. Kilahama**



AWALI ya yote, ni vyema na haki kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyemuweza wa yote na mwingi wa rehema. Yeye ndiye chimbuko letu hadi tukajikuta ni

Watanzania, maana hakuna aliyepiga kura kuchagua awe mwananchi bali ni kwa mapenzi yake.

Kabla ya kutawaliwa na wakoloni, watu katika Afrika, waliishi kama ndugu wakitambua maeneo waishiyo na kuyamiliki.

Historia inaonyesha kuwa mataifa ya kwanza kufika Afrika, ni ya kutoka sehemu za Mashariki ya Kati, hususani taifa la Oman. Watawala wa Oman wakawa wa kwanza kukanyaga maeneo katika Afrika Mashariki, hususani Zanzibar, Bagamoyo, Dar es Salaam, Kilwa-Masoko. Vilevile, walifika sehemu za Mombasa na Malindi nchini Kenya.

Kadhalika, historia inaonyesha kuwa wafalme wawili katika karne ya saba, walitoka Oman wakaja Afrika wakafikia Kisiwa cha Pate karibu na Lamu nchini Kenya.

Pia, inasadikiwa kuwa kati ya karne ya nane na 10, baadhi ya Waarabu kutoka Shiraz,

walihamia eneo la Afrika Mashariki visiwani Zanzibar.

Tena, Sultani wa Shiraz na wanawe wa kiume sita pamoja na wafuasi wao, wakafika Kisiwa cha Pemba na baadhi yao wakaenda kukaa Kilwa-Masoko na wengine Mombasa nchini Kenya.

Baada ya wageni hao kukaa maeneo ya pwani, mwingiliano kati ya jamii ya Kiarabu na wenyeji wa Pwani, ukaongezeka. Hatimaye, kukawepo lugha ya mawasiliano ambayo ni 'Kiswahili' ambacho kimesheheni maneno ya kibantu na 'Kiarabu'.

Kwa sasa Kiswahili ni lugha rasmi ya Tanzania, lakini inayoenea duniani kote kwa kasi kubwa. Hii ni moja ya faida inayotokana na mchanganyiko wa wenyeji na wageni kutoka Uarabuni.

Kwa upande wa Zanzibar, 'Washiraz' walifika na kuwa watawala, lakini pia kukawepo mchanganyiko wa damu za Kiarabu na Kibantu kupitia kuoana na kuimarisha mahusiano kati yao kama 'nguvukazi' ya ziada.

Licha ya kuwepo wageni kutoka Uarabuni na kufanya waliyoyafanya kabla ya ujio wa wageni wengine kutoka Ulaya, Afrika ilikuwa na mifumo yake. Vilevile, wakazi wake sehemu mbalimbali za Bara, walikuwa wakiishi kwa taratibu walizojiwekea.

Enzi hizo hapakuwepo na mataifa yaliyofahamika kuwa na mipaka halisi kama ilivyo sasa; maana Afrika imegawanywa kwenye mataifa 54 yenye mipaka kamili na kila nchi ina mipaka yake, utawala na kutambulika kimataifa.

Chimbuko la mataifa ya Afrika ni enzi za wakoloni walipoingia Barani Afrika na kugawana maeneo ya kutawala na hatimaye kuyawekea mipaka. Tanzania wakati ule, ilijulikana kuwa ni Tanganyika (Bara) na Zanzibar (Visiwani).

Wakati huo, Tanga ilikuwa ni mji (sasa Jiji) kwenye sehemu ya mwambao Kaskazini mwa Tanzania. Hivyo, wakazi wake kwenye ukanda wa Pwani (Waswahili), walikuwa wakiona nchi kavu (ardhi) kutoka pwani hadi upeo wa macho yao. Hali hiyo ilimaanisha kuwa kuna

kilometa nyingi za ardhi, mapori na makazi ndani ya nchi, mazingira ya aina hiyo yakapelekea kujulikana ni 'nyika'. Hivyo, hali-hiyo ikamaanisha kuwa ni 'ardhi' iliyofunikwa na uotoasilia ikiwemo nyasi, mimea mbalimbali pamoja na sehemu zenye maeneo yaliyofunikwa na misitu/mapori pamoja na kuwepo makazi ya watu bila kusahau wanyamapori. Wageni kutoka nje ya Afrika walipofika ukanda wa pwani husasni sehemu za Tanga, wakasikia kuwa kuna 'nyika' kutoka Tanga kilomita nyingi kuingia ndani ya Afrika.

Hivyo, ilitokea kuwa wakati wa kugawana mataifa ya kutawala, wakoloni wakaita nchi iliyotawaliwa na Wajerumani kuwa ni "Tanganyika". Jina hilo lilimaanisha muunganiko wa maneno mawili: 'tanga' na 'nyika' kuwa neno moja: "Tanganyika" (the land beyond Tanga).

Baada ya Vita ya Kwanza ya Dunia kumalizika mwaka 1918; "Tanganyika" ikawa chini ya Waingereza hadi ilipopata uhuru Desemba 9, 1961.

Wasomaji wa Makala hii tujiulize, je, ni kitu gani kiliwasukuma wakoloni kuja Afrika zaidi ya miaka 300 iliyopita? Vilevile, tujiulize ilitokeaje wakaweza kusafiri masafa marefu kutoka Uarabuni na/au Ulaya hadi kufika Pwani za Mashariki na Magharibi mwa Afrika?

Mwandishi siyo mtaalamu wa masuala ya historia au mambo ya nyakati zilizopita; lakini kwa kuzingatia uhalisia na kwa kudadavua hali ilikuwaje tangu wakati ule hadi sasa; nathubutu kusema wakoloni hawakuja kwa nia ya kuiendeleza

Afrika na watu wake. Kimsingi, walikuwa na 'ajenda yao maalum' kama itakavyofafanuliwa kwenye sehemu zote (tano) za makala hii.

Kadhalika, ifahamike kwamba wakati wageni wamekuja Afrika mathalani, Waarabu toka Mashariki ya Kati kuanzia karne ya saba na Wazungu kutoka Ulaya hususani, Wareno tangu karne ya 14, hali inaonyesha kuwa walikuwa wamekwisha kujijengea uwezo kiasi cha kuwezesha kusafiri kupitia baharini kwa kutumia merikebu na/au mashua. Kwa mazingira hayo, inaashiria kwamba kwa kiasi fulani, walikuwa wamefikia kiwango kikubwa cha maendeleo kusudiwa.

Wengi wetu hatuelewi hali ilikuwaje barani Afrika wakati huo takribani miaka 300 au zaidi iliyopita; ingawa kwa baadhi yetu wanaweza kuhisi hali ilivyokuwa kutokana na mapokeo kupitia simulizi za mababu waliotutangulia. Tujiulize, je, kwa wakati huo wakoloni walipojipenyeza wakaingia Afrika walikuta hali ikoje?

Kwa vyo vyote vile, walikuwepo wenyeji wa Afrika, ambao hali yao ilikuwa ya kawaida wakiwa wakulima, wafugaji na wawindaji.

Hata hivyo, wageni kwa mfano, waliotoka Oman wa kwanza kufika Kilwa-Masoko, mkoani

Lindi karne ya saba, wakafuatiwa na Wareno, mfano, (Vasco da Gama) na wengine kama Christopher Columbus, (Mtaliano) walijulikana kama wavumbuzi (explorers) na kufika sehemu mbalimbali za Afrika kupitia Bahari ya "Atlantic" hadi kufika Rasi ya Tumaini Jema (the Cape of Good Hope), Afrika Kusini katika karne ya 14 na kuelekea India na Amerika: Kusini, Kati na Kaskazini hadi Canada.

Historia inaonyesha kuwa wakati huo, wageni wakawa wanashughulika na biashara ya watumwa waliopelekwa Uarabuni na wengine kwenda

Amerika ya Kusini nchini Brazil na sehemu za Caribbean na Amerika ya Kati na USA.

Kadhalika, kati ya karne ya 14 na 18 mataifa kadhaa ya Ulaya ikiwemo, Ufaransa, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na nchi nyinginezo walikuwa wameishajenga 'msingi' mzuri wa kujihakikishia maendeleo ikiwemo mapinduzi ya kiuchumi (viwanda), kisiasa, kiutawala na kitamaduni. Wakati huo maeneo mengi Afrika hasa sehemu za Kati, Magharibi, Mashariki na Kusini; maisha yalikuwa ya kawaida kijamii, kiutamaduni na kabila mbalimbali zikitawaliwa na watemi/machifu.

Katika mazingira hayo, Ulaya na Amerika wakawa na uwezo wa kufanya mambo mengi kujiletea maendeleo kwa kujiamini zaidi. Hata hivyo, mataifa ya Ulaya baada ya kupata taarifa muhimu kutoka kwa 'wavumbuzi na/au

Wamissionari, mathalani, Vasco da Gama na wenzake kutoka Ureno katika karne ya 14 biashara ya watumwa ikashamiri.

Kadhalika, wageni wengine mathalani, Johann Ludwig Krapft na Johannes Lebmann kutoka Ujerumani walikuja Afrika Mashariki mwaka 1846 (miaka 177 iliyopita).

Wajerumani hao walikuwa wa kwanza 'kujidai' kuvumbua Mlima Kilimanjaro na Mlima Kenya.

Baadaye wakafuatiwa na wengine kutoka Uingereza ambao walitembelea maeneo mengi ya Afrika Mashariki na kwingineko hadi Zimbabwe kwenye maporomoko makubwa ya maji (Vitoria falls). Waingereza hao ni pamoja na Sir Richard Burton, John Hanning Speke, na David Livingstone na wengineo. Wakijulikana ni 'wavumbuzi/wamissionari' waliokuja Afrika, kati ya karne ya 17 na 18; wakaona Afrika imesheheni rasilimali watu wengi pamoja na maliasili za kutosha. Hivyo, wakajipanga kwa namna ambavyo mataifa yao yanaweza kunufaika kutokana na rasilimali watu na maliasili walizoziona Afrika.

**Itaendelea sehemu ya 2.**



Paul Mng'ong'o

KLINIKI YA FIKRA

Simu: 0676055444 Email: mngongopaul@yahoo.com

# Mambo ambayo watu wenye nguvu ya akili hawayafanyi-2

KAMA tulivyoelekeza wiki iliyopita, yapo mambo ambayo watu walio na busara na nguvu ya akili, hawayafanyi kwenye maisha yao. Na kuyaacha mambo hayo, ndiyo kunasababisha wasonge mbele kwa haraka. Bahati mbaya ni kuwa, wenye nguvu ya kuyaacha haya ni wachache kwenye jamii zetu. Wengi wanashindwa kuyaacha mambo haya na kujikuta wakiendelea kuishi maisha ya chini siku zote. Mambo haya nayaelezea kifupi kama ifuatavyo: -

**4. Hawahangaishwi na vitu wasivyoviweza kudhibiti**

Mara nyingi tumefikiri kuwa tunaweza kudhibiti kila kitu kibaya kutokea. Ndiyo maana tumepoteza muda mwingi kujaribu kuzuia au kujihusisha na mambo ambayo hatuna uwezo wa kuyadhibiti au kuyabadilisha. Mfano, linatokea jambo au hali fulani kwa mwenzako na mnapishana kabisa. Unatamani aachane na msimamo wake awe vile unavyoona wewe.

Kimsingi mwenzako ana maisha yake na anafikiri na kutenda vile atakavyo. Tunaruhusiwa kujaribu kushauriana na kuelimishana, lakini misimamo ya watu ni nje ya uwezo wetu kudhibiti au kuwabadilisha.

Ikifika mahali umejitahidi kudhibiti hali fulani, lakini uamuzi si wako, lazima utambue kuwa kuna maeneo huna nguvu kudhibiti au kubadilisha mambo na hivyo uwe na amani na kukubaliana na matokeo ili uwekeze nguvu, muda na rasilimali nyingine kwenye vitu mbadala ambavyo una uwezo navyo.

**MKimsingi mwenzako ana maisha yake na anafikiri na kutenda vile atakavyo. Tunaruhusiwa kujaribu kushauriana...**



Jambo kubwa ni kutumia nguvu, ubunifu, uwezo, ushawishi na rasilimali inavyotakiwa ili kufanikihawa, lakini ikatokea nje ya uwezon wako kuna mambo hayaendi na yamegoma, ukatumia kila aina ya nguvu na ikashindikana, usipoteze muda kuendelea nalo kichwani kunung'unika au kulazimisha sababu si kila kitu unakiweza.

Jambo la kwanza kwenye hali kama hiyo, mwachie Mungu anaweza kuanzia hapo kukusaidia au kubali matokeo ili uhamishe nguvu na muda kwenda kwenye mambo mengine. Kuendelea kuhangaikia na mambo usiyoyaweza au kulazimisha vitu ambavyo huwezi kuvidhibiti, kunakutelea madhara mengi kama vile, kusababisha wasiwasi kuongezeka, kunapoteza muda na nishati, kuharibu mahusiano, utawahukumu wengine kwa ukali, utajilaumu bure kwa kila kitu, n.k.

Kwa mfano, unaendesha gari na unawahi kwenye mkutano, unakuta foleni kubwa ya magari ambayo haitembei kabisa, kulalamika, kupiga honi, kutukana, hakusaidii chochote. Badala yake angalia njia mbadala ya kufanya kama unaweza kupata mtu akachukua pikipiki akabaki kwenye gari na kwa pikipiki hiyo wewe uwahi kikao au kama kuna njia nyingine, geuza gari, n.k. Mara nyingine njia bora zaidi ni kuwahi mapema zaidi au kutumia usafiri wa umma ambapo ikitokea umekwama, unaweza kutafuta pikipiki au njia mbadala.

**5. Hawahangaiki kuwapendeza watu wote.**

Kuwajali watu wengine na kutaka kutekeleza fikira zao, kutakuwa gereza lako daima. Utakumbuk kuwa, kwenye jambo la pili tulijadili kuhusu kutoa mamlaka yako kuruhusu watu wengine kudhibiti jinsi unavyojisikia; sasa kwa upande mwingine, kutaka kuwafurahisha watu, ni kujaribu kudhibiti jinsi watu wengine wanavyojisikia.

Jambo hilo litakuumiza wewe na kamwe hutaliweza.

Watu wenye nguvu ya akili hawafanyi jambo hilo kabisa. Kujaribu kuwa mtu mzuri kwa watu wote, kunaweza kuwa na madhara wakati ambao unafikia mpaka wa kuwafurahisha wote. Itakuathiri na kukukuletea ugumu kufikia malengo. Ni muhimu kujua kuwa, unaweza kuwa mtu mwenye upendo na ukarimu bila kujitesa kuwafurahisha wote.

Baadhi yetu hujitahidi kujenga sifa ya kuwa mtu anayekidhi mahitaji ya watu. Tunaona kama thamani yetu huchangiwa na jinsi tunavyowafanya wengine wawe na furaha, matokeo yake hujikuta katikati ya mzozo kuhisi kukataliwa au kupoteza mahusiano. Mara nyingi sababu za watu kujikuta wanapenda kuwafurahisha wengine ni woga wa kukataliwa (fear of abandonment) na kuogopa kutopendwa, au inaweza kuwa mtu kujifunza toka kwa watu waliomzunguka tabia hiyo (Learned

Behaviour), aibu au udhaifu wa kutoweza kusema `HAPANA n.k.

Watu wengi hawajui kuwa mtu ambaye ameishinda tabia hii ya kuishi kwa kuwafurahisha wengine, huonekana imara na mwenye majukumu na malengo kuliko mtu ambaye anajitahidi kuwafurahisha watu ambaye huonekana dhaifu na asiye na mwelekeo.

**6. Hawaogopi kuamua na kuchukua hatua**

Maisha haya hayahitaji woga. Watu wenye nguvu ya akili hufanya maamuzi na kuchukua hatua haraka.

Kwenye maisha tunakabiliana na mazingira ya namna mbalimbali.

Kama ya kifedha, kimwili, kihisia, kijamii na hatari za biashara kutaja chache. Mara nyingi watu huepuka kuchukua hatua kwenye maamuzi magumu yanayoweza kwel kumletea shida. Wakati hisia zetu zinakosa aina yoyote ya msingi wa busara na kujikuta tunaruhusu hisia zitawale hata dhidi ya tathmini za watu maalum. Hisia hizo zitatawala na badala ya kufikiria "kinachoweza kuwa . . ." tunazingatia juu ya vipi kama......";

**Itaendelea wiki ijayo...**



Na Hamisi Kibari
Mtanzania wa kwanza kushinda Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu

# Niko tayari kwa kifo - 8

**Kwa kunogewa penzi la Joyce, Chris anatelekeza familia. Mkewe anapoamua kwenda kwao kulalamika, Chris anahamia nyumbani kwake na hawara yake huyo ili kupunguza gharama za kuishi hoteli. Mkewe anaporejea ghafla kunatokea mtafaruku baina ya mkewe na hawara, hali inayosababisha mfanyabiashara huyo anayeendesha duka kubwa la mbao ampige mkewe hadi kuzirai. Chris analazimika kumpeleka hopsitali. Sasa ameapata ugeni mzito ghafla, hajui pa kuanzia.**

Chris alifungua mlango wa chumba cha daktari kama mtu aliyefukuzwa. Uso wake ulikuwa na mashaka makubwa. Kijasho chembamba kilikuwa bado kinamtoka, kikitiririka hadi makwapani. Mdomo wake ulikuwa umemkauka ghafla kwa kupoteza maji. Njiani alinusurika mara mbili kugongwa na gari kwa jinsi alivyokuwa amechanganyikiwa.

Daktari alimkaribisha: "Karibu Mr. Magati. Umejitahidi kuchunga muda kwa sababu baada ya nusu saa tutakuwa na kikao."

"Ndugu yangu, toka nilipopata simu yako nimechanganyikiwa. Sijui utanisaidiaje kuhusu hili. Ni kweli ulichoniambia?"

"Kaza moyo ndugu yangu. Ninafahamu jinsi ilivyo ngumu kuamini."

"Sasa tufanyeje. Naomba ushauri wako kwa sababu hili ni janga limenipata. Ni janga kubwa."

"Hakuna cha kufanya zaidi ya kwenda kumzika mkeo na sasa pia ujiandae tu kupambana na serikali."

"Kwa nini unasema hivyo?

"Kwa sababu sina namna ya kuendelea kukusaidia baada ya hili kutokea. Itabidi tu ubebe msalaba wako. Maiti itafanyiwa post-mortem na daktari wa polisi, hata tukidanganya kwamba alipata ajali daktari atagundua tu kwamba alikufa kwa kipigo. Sitaki kuharibu kazi yangu. Nilikuwa tayari kukusaidia kama asingefariki dunia. Madhali hilo limetokea msaada wangu pia umekoma," alisema daktari huyo wa chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu, maneno yaliyokuwa yanamchoma Chris moyoni mithili ya mkuki wa moto.

Chris alibaki amemtumbulia macho. Aliona kama daktari amemsaliti licha ya kula pesa zake ili kukwepesha suala hilo lisifike polisi kama tatizo la kipigo bali ajali. Sasa mbona anamtosa 'mazima?'

"Ndugu yangu mbona umenitosa?" Alihoji Chris midomo yake ikiendelea kukauka.

"Kwani ulitaka nifanye nini tena, ndugu?"

"Nilitaka sasa unisaidie kitu kimoja. Ndugu zake niliwaambia kwamba sijui alipo. Nataka pia isijulikane mimi ndiye niliyemleta hapa hospitali na hivyo nikitoka hapa nakwenda kutoa taarifa polisi kwamba mke wangu hajulikani alipo. Hilo tu ndugu yangu. Yaani nimechanganyikiwa."

"Ninashauri kwa sasa ungewaambie tu ukweli, ndugu."

"Loh! Ndugu zake hawataelewa kitu. Siyo siri naweza kujikuta kwenye matata makubwa. Kwanza wakiunganisha nukta kuhusu niliyowaambia kwamba aliondoka na sijui alipo, hawataweza kuamini kwamba sikudhamiria kumuua nilipompiga. Watajiuliza kwa nini sikusema ukweli tangu mwanzo nah apo ndipo balaa litakapoanzia... Yaani sijui nifanyeje. Nisaidie bwana daktari."

"Unataka nikusaidieje Mr Magati?"

"Mbona nimeshasema? Nimekwambia kwamba ndugu zake nimewaeleza kuwa sijui alikokimbilia. Jana ilikuwa tufanye kikao na baba yake, kwani bado yuko hapa mjini. Tukikubaliana kwamba tuendelee kumtafuta na leo nimeshapigiwa simu nyingi sana lakini sipokei. Nisaidie ndugu yangu, Nataka ionekane kwamba mke wangu Tausi si mimi niliyemleta hapa. Shida haina mmoja, nisaidie la jua na mimi pengine kuna siku nitakufaa la mvua."

"Kwa hiyo ulikuwa humpendi mkeo kiasi hiki? Hata kama mzika hutaki. Mbona nikimwambia hata kama amekufa anaonekana mwanamke mrembo sana."

"Hapana dokta. Mke wangu ninampenda na nilimpiga kwa sababu ya hasira tu. Nadhani ni shetani tu. Lakini kwa jinsi hali ilivyo, ninaona njia nzuri ya kukwepa haya matatizo na sintofahamu niliyoisababisha mimi ni mke wangu kubaki kitendawili mahala alipo. Nina hakika hii siri itabaki kuwa kati yangu na wewe."

"Unachopasa kujua ni kwamba, kabla hajafariki dunia, kesi yako kama ingefikishwa polisi ilikuwa ya kudhuru mwili kama sikosei, lakini sasa ni ya mauaji. Siwezi kujiingiza huko kirahisirahisi labda kama utakubali masharti yangu."

**"Mbona nimeshasema? Nimekwambia kwamba ndugu zake nimewaeleza kuwa sijui alikokimbilia. Jana ilikuwa tufanye kikao na baba yake, kwani bado yuko hapa mjini. Tukikubaliana kwamba tuendelee kumtafuta na leo nimeshapigiwa simu nyingi sana lakini sipokei. Nisaidie ndugu yangu, Nataka ionekane kwamba mke wangu Tausi si mimi niliyemleta hapa. Shida haina mmoja, nisaidie la jua na mimi pengine kuna siku nitakufaa la mvua.**

"Niko tayari Dokta. Yamenifika shingoni. Niko tayari."

"Sikiliza Mr Magati, nilijua hili litakuwa tatizo kwako na ndio maana nimekuita ili nione mtazamo wako kabla sijathibitisha rasmi kifo cha mkeo. Baadaye tutakuwa na kikao ambako taarifa zote za matukio ya tangu jana zinatakiwa kutolewa."

"Kwa hiyo utanisaidiaje."

"Huko ndiko ninaelekea. Hebu nisubiri dakika mbili tatu. Ninakuja nione namna ambavyo nitakusaidia," alisema daktari hiyo kijana bado akinyanyuka na kutoka nje kwenye ofisi yake. Alimkadiria kuwa na umri kati ya miaka 25-30.

Chris alibaki kwenye ofisi ya daktari akiwa na mawazo mengi. Hakujua atakabiliana vipi na kifo cha mkewe ambaye kwa takribani siku nne, alikuwa bado yuko kwenye chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu.

Daktari alichukua muda mrefu hadi Chris akaingia na wasiwasi. Aliporejea alimwambia kwamba ili ionake marehemu hana ndugu na kufanya mpango wa harakaharaka wa kuzikwa na halmashauri zinatakiwa Sh. milioni 50.

"Hili ni jambo nitakalowahusisha watu ziaidi yangu vinginevyo jela haitokuacha kwa kuua bila kukusudia. Katika hali mimi sitakuwa tayari ku-risk kibarua changu hivihivi. Kwa hiyo kazi ni kwako. Ukubali kukabiliana na vyombo vya sheria kwa mauaji au tumpoteze mkeo hadi maiti yake. Hakuna atakayejua lolote na habari zake zitabaki kuwa kitendawili kitakachokosa mtu wa kukifumbua. Tukikubaliana, utakachofanya, utaanza kumtafuta mkeo kwa kufungua polisi jalada la mkeo kupotea, kisha utaanza kumtafuta hadi hapa hospitali na maiti yake haitaonekana kamwe."

Chris alibaki mithili ya mtu aliyepigwa shoti ya umeme. Alijiuliza Sh milioni 50 angezipata wapi wakati ndio ulikuwa mtaji wake wa biashara na hapo bado alikuwa na deni la Benki.

"Ndugu yangu, hicho kiasi ni kikubwa sana. Hata ukisema nusu yake tu bado ni kubwa kwangu. Hebu angalia namna ya kunisaidia."

"Hili ni jambo ambalo litawahusisha watu wengi wakiwemo polisi... Ningekuwa wewe, kama nina nyumba ningeuza ili nizime hili jambo. Otherwise, kama unataka kuchezea jela basi, ngoja tufanye utaratibu uchukue maiti ya mkeo ukazike."

Chris alibaki ameduwaa. Alikuwa na maswali mengi kichwani kuhusu mustakabali wa kifo cha mkewe asijue afanye nini.

***

Ilikuwa siku ya Jumapili, Mwalimu Misango alikuwa yuko uani akifua nguo kwa kushirikiana na msichana wake aliyekuwa alimsaidia kazi za ndani. Mlango uligongwa na Jacob, kaka yake Mama Kenny akaingia. Walisalimiana. Mama Kessy akamkaribisha kiti pale uani. Akaacha kufua na kwenda kumsikiliza mgeni wake.

"Samahani Mwalimu, imebidi nikutembelee asubuhi asubuhi kwa sababu hali ya kutoonekana kwa dada inazidi kunitia wasiwasi. Nimepeleleza kwa ndugu zetu wote hapa mjini, na wale wa mikoani nimepiga simu kwa ndugu wote. Lakini hakuna mwenye taarifa zake. Nimempigia tena shemeji Chris akanijibu kwamba bado dada hajarudi nyumbani. Nimemuomba tukatoe taarifa polisi anasema twende kesho. Jana pia aliponiambia hajamwona akaniambia angekwenda kutoa taarufda poilisi. Sasa kesho inazaa kesho na Mzee Chitawo anazadi kuwa na wasiwasi... Nilikuwa nimeshaamua niende polisi peke yangu, lakini nikaona nije kwanza kusikia ushauri wako."

Mama Kessy ambaye alikuwa ameketi kwenye stuli kumsikiliza mgeni wake huku povu la sabuni likiwa halijakauka kwenye mikono yake, alibaki kimya akitafakari maneno yale.

Jacob akamgeukia tena, "Unajua mwalimu, yule mdogo wangu ninamfahamu. Ana roho nyepesi. Wakati fulani alikorofishana na shangazi aliyekuwa akiishi pale nyumbani kwa Mzee Chaitawo akatishia kunywa sumu ili kujitoa uhai. Tendo la kuletewa hawara ndani, tena chumbani mwake, anaweza kabisa kujinyonga."

"Hilo mimi silifikiri sana. Kwanza tungeshapata habari tangu alipotoweka, leo siku ya tano, siyo? Tungesikia redioni au kusoma magazetini. Lakini suala la Polisi sasa ni muhimu."

*Itaendelea*

# Vichanga na wagonjwa wafa kwa kukosa oksijeni



**GAZA, Palestina**

MENEJA wa Hospitali muhimu ya Al-Shifa mjini Gaza, Dk. Mohamed Abu Selmia, ameambia BBC kuwa watu 32 wamefariki dunia katika siku za hivi karibuni.

Dk. Selmia alisema watoto watatu waliozaliwa kabla ya wakati (njiti) na watu saba, walikufa kutokana na ukosefu wa oksijeni, alisema.

Alisema wagonjwa wengine kadhaa wanaohitaji tiba ya figo ya dialysis kwa dharura, wanatarajiwa kufariki duni siku chache zijazo kwani matibabu hayapatikani tena.

"Hospitali inakaribia kukosa mafuta na rasilimali nyingine ili kuendelea kufanya kazi huku watoto wachanga waliozaliwa kabla ya muda, wakiwa wametolewa nje ya vifaa maalumu vya kuwatunza (incubators) ambavyo havifanyi kazi tena. Kuna zaidi ya wagonjwa 600 waliojeruhiwa pia," alisisitiza Dk. Selmia.

BBC ilimuuliza daktari iwapo Jeshi la Israel lilikuwa na mawasiliano yoyote kuhusiana na kuwahamisha wagonjwa au watoto wanaozaliwa kabla ya wakati.

Israel imesema kuwa imetuma mafuta karibu na hospitali na rasilimali nyingine.

Lakini daktari alisema: "Hapana, hawajafika, badala yake tuliwasiliana nāo ... lakini mpaka sasa hatujapata majibu."

"Kuna mazungumzo kuhusu kuwahamisha watoto wanaozaliwa kabla ya wakati, lakini mpaka sasa hakuna kilichofanyika."

Dk. Selmia alisema hospitali hiyo pia imewasiliana na Shirika la Msalaba Mwekundu ili kujaribu kuratibu mazishi ya miili hiyo, ambayo ilikuwa takriban 150 katika hospitali hiyo, lakini iliambiwa kwamba kwa sasa haiwezekani.

BBC.

# WHO: Hospitali Kuu ya Gaza yageuka makaburi

**GAZA, Palestina**

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeielezea Hospitali ya Al Shifa kuwa inageuka kuwa makaburi.

Msemaji wa WHO, Christian Lindmeier, alisema takriban watu 600 wamekwama ndani ya hospitali hiyo na miili ya watu inarundikana ndani na nje ya hospitali hiyo kubwa zaidi Gaza ambayo Israel hairuhusu isafirishwe kuzikwa au kuhamishwa kwa vyumba vya kuhifadhia maiti.

Madaktari wa hospitali hiyo wanaonya karibu shughuli zote zimekwama, mbwa wameanza kuingia hospitalini humo kula maiti, wagonjwa wa figo wakishindwa kupata matibabu maalum na maisha ya watoto njiti yakiwa hatarini kwani umeme umekatwa.



**Pamoja na Al-Shifa, hospitali nyingine katika Ukanda wa Gaza zimeripoti masuala yaliyoenea, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vifaa na nguvu kwa sababu ya mapigano...**

Dk. Mohamed Abu Selmia, aliambia BBC kwamba kwa vile mamlaka ya Israel bado haijatoa kibali kwa miili iliyoharibika kuondolewa hospitalini kuzikwa, mbwa sasa wameingia katika uwanja wa hospitali na kuanza kula maiti.

Mark Regev, Mshauri Mkuu wa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alisema Israel ilikuwa ikitoa suluhu la vitendo kuwahamisha watoto hao wachanga na kuwashutumu Hamas kwa kutokubali mapendekezo.

Pamoja na Al-Shifa, hospitali nyingine katika Ukanda wa Gaza zimeripoti masuala yaliyoenea, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vifaa na nguvu kwa sababu ya mapigano na vikwazo vinavyotekelezwa na Israeli katika eneo hilo tangu Hamas ilipoanzisha mashambulizi yake kwa Israel Oktoba 7, mwaka huu.

BBC.

# Ndege yapotea njia, yagonga gari barabarani

**WASHINGTON, Mareani**

NDEGE ndogo ya propel, imeshindwa kutua kwenye njia yake ya kawaida na kutua kwenye uwanja wa ndege wa Texas na badala yake ikapita katika barabara na kugonga gari lililokuwa likipita barabarani.

Picha ya video ya tukio hilo iliyochukuliwa na mtazamaji, Jack Schneider, ilionyesha ndege hiyo ikianguka kwenye uzio wakati wa kutua kwa dharura.

"Niliona ndege ikishuka kwenye njia ya kurukia ndege haraka nikajua kwamba hakuwa na wakati wa kusimama," Schneider aliliambia Shirika la Habari la WFAA-TV mwishoni mwa wiki, na kuongeza:

"Ni wazi ilikuwa ikienda kasi sana, matairi yalikuwa yakifuka moshi."

Dereva wa gari hilo alipelekwa hospitalini akiwa na majeraha madogo, huku watu wawili waliokuwa ndani ya ndege, wakiwa salama bila majeraha.

Utawala wa Shirikisho la Usafiri wa Anga unachunguza sababu ya ajali hiyo.

BBC.

# Hamas lawamani kwa kuigeuza hospitali Al-Shifa eneo la vita

**YERUSALEM, Israel**

MSHAURI Mkuu wa Waziri Mkuu wa Israel, Mark Regev, amedai kuwa Hamas ndiyo wa kulaumiwa kwa kugeuza hospitali ya Al-Shifa - kubwa zaidi huko Gaza, kuwa eneo la vita.

Katika mazungumzo na BBC, alisema Hamas imejenga kwa makusudi miundombinu ya kijeshi chini ya hospitali hiyo na imewatumia watoto hao kukinga mashine zake za kijeshi.

Hata hivyo, Hamas na maafisa wa hospitali, wamekataa mara kwa mara madai hayo yanayohalalisha mashambulio ya Israel karibu na hospitali za ukanda huo. Regev alidai kuwa Israel haikujadili kulenga hospitali.

Alisema Hamas walitaka picha zionyeshe shida na hawakuwa tayari kukubali suluhisho la mafuta ili hospitali iendelee kufanya kazi.

BBC.



## Kusambaratika kwa Empire Bakuba

# Elvis Kunku: Lofombo, Bileku walidekezwa na Pepe Kalle

## ■ Awataja watoto walioachwa na Pepe Kalle
## ■ Amkana Alain Kabasele wa Akudo Impact



Elvis Kunku

**KATIKA mfululizo wa makala hizi za ilipo Empire Bakuba, UELEKEO ilizungumza na wanamuziki wanne waandamizi katika kundi hilo. Haya yalikuwa ni mahojiano ya kwanza kufanywa na wanamuziki hao juu ya uhai wa bendi hiyo tangu kufariki kwa aliyekuwa mmiliki mkuu Kabasele Nyampanya 'Pepe Kalle'. Pepe Kalle alifariki Oktoba 28, 1998. MWANDISHI WETU PETTER MWENDAPOLE anaeleza.**

GAZETI hili lilianza kuchapisha mahojiano wiki iliyopita, ambapo Bileku Mpasi alieleza uwepo wa bendi hiyo lakini ikiwa haina nguvu na kisa kilichowafanya wao kuondoka ni tamaa ya fedha ya viongozi wao, Dilu Dilomona na Papy Tex.

Katika toleo hili tuna majibu ya Elvis Kunku aliyekuwa mpiga solo na rythim, na wiki ijayo tutahitimisha makala hizi kwa mahojiano na watu wawili Gode Lofombo mpiga bass na Papy Tex ambaye alikuwa na hisa kwenye bendi na mwimbaji kiongozi. Mwanahisa mwingine Dilu hatukuweza kumpata. Endelea…

"Empire Bakuba bado haijafanya ipo na inafanya maonyesho kama kawaida…na tumetoa albamu kadhaa tangu mwaka huo 1998 baada ya kifo cha Pepe Kalle," anasema Kunku.

Anasema wengi wanadhani bendi hiyo haipo tena lakini wameweza kufanya onyesho jijini Kinshasa ukiwa ni mwaliko wa Serikali ya Rais Joseph Kabila.

"Rais wa bendi Dilu Dilomona alikuwepo, Papy Tex alikuja kutoka Uswisi anakoishi, Djodjo Ikoko, Doris na vijana wengine wote walikuwepo tukafanya onyesho," anasema.

Kunku anasema yeye ni mmoja waanzilishi wa bendi hiyo waliyoitengeneza Machi 17, mwaka 1972. Anasema waanzilishi walikuwa yeye, Jean Baptiste Kabasele Yampanya 'Pepe Kalle', Dilu, Papy Tex, Jeff Tumba, Maitre Cherie, Bilandu, Babalu, Mali Muzita (mpiga Drum), Saka (Trumpet), Benazo (Saxaphone), Likinga Nzingangole, Dorice, Kokongasi na Jeff Lunyama.

Anasema marehemu Luambo Luanzo Makiadi 'Francoo' na Kiamanguana Kiamateta 'Verkys' ndio walikuwa wafadhili wa bendi hiyo na mwaka 1981, Verkys alilipia bendi nzima nauli kwenda Ulaya kwa ajili ya kurekodi.

Mzee huyo ambaye bado anafanya muziki anasema baada ya kifo cha Pepe Kalle walifanya kikao cha pamoja kujua muelekeo wa bendi.

"Cha ajabu bwana mdogo, Lofombo akasimama na kusema kwamba yeye hawezi kufanya kazi na wazee wakati vijana wenzake huko nje wanajitegemea…huyu bwana mdogo alijisahau kuwa ujuzi aliokuwa nao ameupata wapi, mpaka asimame mbele yetu na kutoa kauli hiyo.

"Unajua hawa vijana Djouna Mombafu (Bileku Mpasi), Emoro na Lofombo walidekezwa sana, hata wakati Pepe Kalle yupo, kama ikitokea amechelewa kufika basi nao hawapandi jukwaani watakuwa wanajizungushazungusha, ilifika wakati waliona kama bila wao bendi haitaendelea." Anasema.



Bileku Mpasi

Kunku anasema kikao Bileku na Lofombo waliamua kundoka na kuunda Delta Force ambalo halikuchukua muda likasambaratika kwani walipigana wao kwa wao mpaka aliyekuwa mdhamini wao kampuni ya bia ya Bralima ikasimamisha mkataba na ukawa mwisho wao.

"Na utaona kuwa Bakuba haikuvunjika, tuliendelea kupiga muziki na kutoa albam kama Fukumwindu (2000), Sovatage (2002), Mone Bebe (2003) lakini pia tuliwahi kufanya onyesho hapa Paris la miaka 10 baada ya kifo cha Pepe Kalle tukatengeneza na albamu iliyoitwa Flashh lakini Producer mmoja mkubwa tu aliamua kutubania," anasema.

Mwanamuziki anasema wanajiandaa kurudia nyimbo kadhaa za zamani za kundi hilo ili zisikike tena kwa wapenzi wao. Akizungumzia ziara anazozikumbuka, Kunku anasema anakumbuka ziara bendi hiyo nchini Tanzania katika onyesho lililofanyika Uwanja wa Taifa.

"Kuna bendi tulipiga nayo Uwanja wa Taifa, Yule mpiga solo wao alikuwa na viwango vingine kabisa, uwezo wake ulikuwa juu, hata mpiga rythim kwakweli alikuwa na uwezo, walinifurahisha sijui wako wapi?"

Kuhusu maisha ya Pepe Kalle na watoto, Kunku anasema mwanamuziki huyo aliacha watoto watano ambao yeye anawatambua na kutokana na ukaribu wake na marehemu.

"Mtoto mmoja ni mwanamuziki yuko na Fabrigas katika bendi ya Villa Nova anaitwa Fiston ni mwimbaji, wengine wawili wanaishi hapa Ufaransa, halafu yuko anayeishi Sweden ambaye alizaa na mcheza shoo wa Mpongo Love, na wa mwisho yupo Ubelgiji akiendelea na shughuli zake."

UELEKEO lilimuuliza kuhusu mtoto aliyepo Tanzania ambaye inaelezwa kuwa mtoto wa Pepe Kalle, Kunku amesema hana taarifa na mtoto huyo, yeye ndiye mtu aliyekuwa karibu na marehemu, wamekuwa wote wakati wa ujana na walikuwa hawafichani vitu, hata baada ya kifo watoto hao wengine wamekuwa wakiwasiliana na yeye.

WIKI Ijayo, msome Abdalah Gama mmoja wa waanzilishi wa bendi ya Mlimani Park Orchestra ambaye kwa zaidi ya miaka 10 iliaminika amefariki na hakuna aliyekuwa akijua alipo. UELEKEO limezungumza nae mambo mengi.



Bileku Mpasi (kulia) akiwa kwenye harusi ya binti yake.





## Kona ya **Urembo**

Na Hidaya Machuppa Simu: +255 765 828 219

# Kwa nini unahitaji kuvaa 'Kawaida'?



MIONGOZO ya nini cha kuvaa unapoenda kwenye ofisi muhimu za mteja au ikiwa umealikwa kwenye hafla ya hali ya juu.

Ukiwa umevalia nadhifu katika koti la chakula cha jioni huonyesha mratibu wa tukio kuwa unamheshimu na unathamini kualikwa.

Matukio au mahali ambapo mwonekano mzuri ni muhimu ni tofauti sana na mipangilio ya faragha, biashara ya 'kila kitu kingine': kugonganisha glasi na bosi kwenye choma nyama, kumtazama mama mkwe wako akizima mishumaa ya siku ya kuzaliwa, au mwaliko usio rasmi. kunywa na baadhi ya wafanyakazi wenzake.

Shujaa Kawaida

Kanuni ya Mavazi ya Kawaida

Huna haja ya tie au suruali kali ya suti kufanya kazi ya kitaaluma:

#### Lakini vazi la kawaida ni la nini?

Mavazi ya kawaida huweka msisitizo juu ya faraja na mtindo wa kibinafsi, kwa kuwa haya ni muhimu zaidi kwa hali hiyo kuliko taratibu.

Kanuni ya mavazi ya kawaida husaidia kuweka mfumo wa tafsiri. Neno 'kawaida' lina maana ya kustarehesha na isiyo rasmi, kwa hiyo mavazi yanafanya kazi sawasawa na ya starehe. Hata hivyo, kujipamba na kiasi kinachofaa cha uzuri ni muhimu tu na kanuni hii ya mavazi.

#### Kanuni za Msingi

T-shirt, jeans na wakufunzi: wote wanaruhusiwa chini ya kanuni ya mavazi ya kawaida.

Flip-flops, kaptula au nguo za begi kama vile suruali ya jasho au kofia hazikaribishwi kabisa. Mipako yenye kubana kupita kiasi ni kichocheo cha usumbufu, ndiyo maana 'kuvaa kwa kawaida' hufunika sehemu zisizo huru, zinazotoshea hewa (inayojulikana kama 'casual fit').Vitambaa kama vile denim, pamba, flana, kitani na polyester ni sifa za kawaida na zinaweza kuunganishwa na vifaa vya kifahari zaidi kama vile hariri na cashmere. Chiffon, brocade na velvet, kwa upande mwingine,

#### Soksi za Kujiamini

Mwonekano wa kawaida hukuruhusu kuonyesha utu wako. Chaguo moja maarufu ni soksi za rangi au muundo ambazo unaweza kuchanganya na rangi katika vazi lako unapochagua.

Kwa kuchukua soksi kama msingi wako, una chaguo nyingi kwa michanganyiko mipya ya mavazi ambayo itaonyesha mtindo wako mahususi kwa hali nzuri ya kujiamini na mguso wa ustadi wa hali ya juu.

#### Kawaida kwa Wanaume

Chaguo mojawapo ni jeans au chinos pamoja na viatu vya kuingizwa na shati nyepesi au sweta ya knitted. Ikiwa unakwenda kwa T-shati, basi mavazi yako yanaweza kufanya kazi vizuri na koti rahisi au blazer. Mahusiano yanaweza kushoto kunyongwa kwa usalama katika vazia. Watu wengine wanaweza kuhisi haja ya kufuata mwenendo wa mtindo, lakini vipande vya classic vinabaki chaguo salama zaidi.



Mitindo inaweza kutoeleweka na kwenda kombo haraka, ikimaanisha kuwa kile kinachokusudiwa kama mkusanyiko wa mtindo wa vipengele vya mtindo hivi karibuni huwa kinyume kabisa. Mavazi bora zaidi ni yale ambapo huwezi kuona ni mawazo mengi yameingia ndani yake, kwani hii inaonyesha kutojali na uthibitisho wa mtindo wa mtu binafsi uliolegeza.

SOCKS NYEUSI ni zaidi ya sahihi. Ikusaidia kwa furaha kupata soksi zinazofaa kwa miguu yako. Kutoka kawaida hadi rangi, pamba hadi cashmere - kwa soksi zinazokufaa zaidi.

#### Je! ni miongozo gani ya kuvaa kwa mtindo huu?

Smart casual ni msimbo wa mavazi ambao unaweza kutofautiana kulingana na mahali pa kazi, kampuni na tasnia. Angalia tu pande zote, haswa kwa viongozi wakuu, ili kuelewa kile kinachofaa.

Smart casual ni ya kitaalamu lakini imetulia kidogo - mavazi ya kifahari zaidi ya nguo za kawaida pamoja na vitu vya kawaida au vya kufurahisha vilivyooanishwa na vipande nadhifu zaidi.

Kwa wanawake, hii ina maana kwamba vitu kama vile suti ya vipande viwili au nguo za ushirika zinaweza kuepukwa.

Ili kuweka mwonekano mzuri wa kawaida, chagua vitu kama vile:

Nguo za juu: blauzi na shati zisizo na upande wowote au za rangi na/au zilizochapishwa, kadi nadhifu katika vitambaa vya kuvaa kama vile knit knit, mashati ya vifungo vya hariri juu au mashati yenye kola. Blazi zilizoundwa vizuri, zinazovaliwa kama suti tofauti badala ya kufanana, pia ni njia nzuri ya kuboresha mwonekano.

Chini: suruali iliyopangwa (chagua kutoka kwa mitindo iliyopigwa, ya moja kwa moja au pana), suruali ya chinonona denim ya safisha ya giza, lakini kumbuka jeans inaweza kuwa au haifai, kulingana na kampuni.

Sketi za midi na sketi za penseli za maridadi (urefu wa goti au chini) pia hufanya kazi vizuri.

Nguo: Nguo maridadi za midi, gauni za kanga, nguo maridadi za penseli na nguo za shati nadhifu za mikanda. Weka nguo kwa urefu wa goti au chini. Epuka nguo za penseli za classic / rasmi.



Viatu: Visigino na tambarare zote zinakubalika kwa mwonekano mzuri wa kawaida. Chagua kutoka kwa ballet mahiri au magorofa yaliyochongoka, lofa au brogu. Kwa visigino, chagua sling-backs, visigino vya kitten, pampu, visigino vya kuzuia, wedges smart na buti za mguu.

Vifaa: Vito vya ujasiri huongeza mguso wako wa kibinafsi lakini kikomo kwa vipande vya taarifa moja au mbili. Au chagua vipengee vilivyosafishwa zaidi na rahisi kama vile pete, bangili na shanga. Skafu za hariri pia huongeza mwonekano mzuri na uliong'aa kwenye vazi.

#### Epuka Makosa 5 ya Juu ya Misimbo ya Mavazi ya Smart Casual

1. Kuvaa nguo za kawaida sana. Ni afadhali sana kuvikwa nguo nyingi kuliko kuvikwa nguo za chini. Epuka kuvaa mavazi ya kawaida, ya wikendi kwenda ofisini kama vile suruali ya mizigo au jogger, nguo za kuelea au ndefu za kiangazi, kofia/skirt ndogo na fulana za picha au nembo.

2. Kuvaa kichwa hadi vidole katika mavazi ya jadi ya ushirika. Hii inaweza kutuma ujumbe kwamba huelewi kanuni ya mavazi au huna uhusiano na mambo muhimu leo. Inaweza pia kuashiria ukosefu wa mtindo wa kibinafsi. Ingawa baadhi ya vitu vya kitamaduni vinaweza kuunganishwa na vitu vya kawaida zaidi, epuka mwonekano wa kampuni uliojaa sana.

3. Kutozingatia sana upambaji wako. Jambo kuu ni kuangalia mtaalamu ili mavazi yako yote, ikiwa ni pamoja na viatu vyako, viwe katika hali nzuri. Hiyo ina maana hakuna madoa yanayoonekana, nyuzi zilizovutwa au zilizolegea, alama za scuff au visigino vilivyovunjika. Nywele na vipodozi vyako pia vinapaswa kuonekana vimeng'aa na nguo hazina mikunjo.

4. Kuvaa yoyote kati ya yafuatayo:

Leggings au kitu chochote ambacho ungevaa kwenye ukumbi wa mazoezi Kamba ya tambi/vifuniko vya juu visivyo na kamba

Vipande vya juu vilivyokatwa ambavyo vinaonyesha wazi kupasuka

Kitu chochote ambacho kinaonekana kwa mbali

Lycra au kitambaa chochote kinachokaza Thongs au flip flops

5. Kuvaa nguo zisizokaa vizuri. Hii inatumika kwa kanuni yoyote ya mavazi, lakini inapokuja suala la busara la kawaida, ni muhimu sana kudumisha mwonekano wa kitaalamu dhidi ya uzembe.

# Rhulani Mokwena, Kocha mdogo mzawa mwenye mafanikio makubwa

KATIKA vichwa vya wapenzi wengi wa soka inaamanika ili timu ipate mafanikio lazima Kocha Ulaya. Klabu nyingi zimelazimika kuwalipa makocha wa kigeni hususani barani Ulaya ili kuzisaidia timu zao.

Lakini Tumewaona Abdalah Kibaden wa Tanzania akiifikisha Simba katika fainali za Kombe la Washindi Baraani Afrika na kushindwa na Stella Abidjan mwaka 1993, Tumemuona Tito Mwaluvanda (Marehemu) akiipeleka Yanga katika hatua ya makundi mwka 1998.

Mwaluvanda ambaye alichukua ubingwa wa Ligi Kuu na Ligi ya Muungano 1998, tena akiweka rekodi ya ushindi mnono zaidi katika Ligi ya Bara, mabao 8-0 waliyoifunga Kagera Shooting Stars (sasa Kagera Sugar), tena ikiwa inafundishwa na kocha wa timu ya taifa, Taifa Stars wakati huo, Zacharia Kinanda 'Arrigo Sachi' (sasa marehemu), Edibilly Jonas Lunyamila akifunga mabao matano peke yake.

Mwaluvanda aliiweka rekodi mbili kuifanya hiyo iwe klabu ya kwanza Tanzania kucheza hatua hiyo, yeye kuwa kocha wa kwanza mzalendo na wa mwisho hadi sasa kuifikisha timu katika hatua hiyo.

Tumemuona Pitso Mosimane akiibuka na kuwa Kocha kinara Afrika na sasa ua jipya limechipuka Rhulani Mokwena.



Abdallah Kibadeni

### Historia yake

Rhulani Mokwena Mzaliwa wa jiji la Johannesburg amezaliwa Januari 9, 1987), Mwana wa mchezaji wa zamani wa Orlando Pirates, Julias Sono, na mpwa wa Jomo Sono.

Mokwena anatoka katika familia ya wanasoka na alianza taaluma yake ya ukocha katika mifumo ya vijana katika timu ya Silver Stars, kabla ya kuhudumu kama meneja msaidizi wa Mamelodi Sundowns na Pirates. Mnamo 2019, alikua meneja wa muda wa pili katika bencHi la ufundi la Mamelodi, akishikilia wadhifa huo kwa miezi mitano, kabla ya kuteuliwa kama kocha mkuu wa Chippa United mwaka uliofuata.

### Walimu wake

Ushindi wa kwanza wa Mokwena katika soka ulikuja katika klabu ya Silver Stars, ambayo baadaye ilijulikana kama Platinum Stars ambayo kwa sasa inaitwa Marumo Gallants. Mokwena aliboresha ujuzi wake chini ya makocha kama vile Steve Komphela, Cavin Johnson na Allan Freese.

Mnamo 2014, alijiunga na Mamelodi Sundowns ambapo, baada ya kufanya vyema katika timu ya vijasna ya klabu hiyo, alipandishwa cheo na kuwa mmoja wa wasimamizi wasaidizi wa meneja Pitso Mosimane, pamoja na Manqoba Mngqithi na Alex Bapela.

Mokwena alikaa na Masandawana hadi 2017, akiisaidia klabu hiyo kushinda taji la Ligi ya Mabingwa ya CAF 2016, kabla ya kuchukua nafasi kama meneja msaidizi wa Milutin Sredojević 'Micho' kule Orlando Pirates.

### Timu alizosimamia Orlando Pirates

Mnamo Agosti 2019, baada ya Micho kujiuzulu Orlandon bila kutarajiwa, Mokwena alitangazwa jwa kama meneja mpya wa muda wa timu na mechi yake ya kwanza ya usimamizi kwa alishinda bao 1-0 dhidi ya Highlands Park.

Katika muda wa miezi mitano iliyofuata, alichukua jukumu la mechi 14, akishinda nne, sare tano na kupoteza tano, kabla ya kurudi kwenye nafasi ya meneja msaidizi kufuatia uteuzi wa Josef Zinnbauer mnamo Desemba.

### Chippa United

Machi 4, 2020, Mokwena aliondoka kwenye kikosi cha Orlando baada ya kuteuliwa kuwa kocha mkuu wa timu ya Ligi Kuu ya Chippa United kwa mkataba wa muda mfupi.

Hata hivyo, muda wake na klabu ulitatizwa na mlipuko wa COVID-19, ambao ulisababisha ligi kusitishwa baadaye mwezi huo, na kufikia mwisho wa kandarasi yake mnamo Juni akiwa amesimamia mechi moja pekee.

### Mamelodi Sundowns

Mnamo 2020 Mokwena alikua mkufunzi mwenza wa Mamelodi Sundowns pamoja na Manqoba Mngqithi. Mnamo Oktoba 2022, Mokwena alipandishwa cheo na Kocha Mkuu wa Sundowns.

Na historia mpya ikaanza kuandikwa kuanzia hapo.

### Mafanikio

Rhulani Mokwena amekuwa akifanya vyema katika kazi yake ya ukocha katika klabu ya Mamelodi Sundowns, kati ya mechi 50, Kocha huyo mwenye umri wa miaka 36 ameshinda michezo 35, sare 14 na kupoteza mmoja pekee. Asilimia 70 ya ushindi kutoka kwa idadi iliyotajwa hapo juu inavunja rekodi iliyokuwa ikishikiliwa na Pavle Dolezar ambaye alisimamia 66%.

Katika mchezo wa mwisho wa Fainali ya African Football League Mamelod Sundowns walishinda 2-0 dhidi ya Wydad Casaablanca na Mokwena alikuwa na mchango chanya sana katika ubingwa huo.

Ndiye aliyepanga mpango mkakati ambao ulishinda shinikizo la mapema la Wydad kabla ya kutumia vibaya makosa na kuwaadhibu bila huruma. Ushindi huo unafikisha ushindi wa kihistoria wa bara kwa Sundowns ambao sasa wamekuwa mabingwa wa kwanza wa Ligi mpya ya Soka ya Afrika (AFL).




Aina ya mpira anaofundisha Mokwena na namna ya muonekano wake nje ya uwanja unavutia kila mtu anaeangalia burudani ya soka lake. Huyu ni Pep Guardiola wa Afrika

Makala hii imendaliwa na Valensi Mbaga kwa msaada wa vyanzo mbalimbali vya habari.



# Neymar kidogo kuna matumaini

**SAO PAULO,Brazil**

FOWADI machachari Neymar amewataka marafiki na familia yake kuwa karibu nae zaidi kufuatia jeraha lake baya la goti akiichezea Brazil mwezi Oktoba.

Neymar anayendelea vizuri kwa sasa baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti alitoa kauli hiyo kupitia akaunti yake ya Instagram. Madaktari wamesema hawajui ni lini fowadi huyo wa Al-Hilal atarejea uwanjani.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 aliumia goti lake la kushoto alipokuwa akiichezea Brazil katika mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia 2026 mwezi uliopita.

Taarifa zinasema aina ya jeraha alilonalo linaweza kuwa miezi nane hadi kumi.

Rodrigo Lasmar, daktari wa timu ya Brazil, alisema Neymar amejitolea kikamilifu kurejesha usawa kamili.Ameonyesha, tangu wakati wa kwanza, kwamba anafuata kile tunachopendekeza.

Neymar alitolewa nje kwa machela huku akilia wakati Brazil ilipochapwa 2-0 na Uruguay baada ya kutua vibaya kufuatia changamoto katika kipindi cha kwanza.

Neymar ambae kwa sasa anakipiga Al-Hilal ya nchini Saudi Arabia msimu wa joto kutoka Paris St-Germain kwa euro 90m (£77.6m) pamoja na nyongeza lakini amecheza mechi tano pekee kwa sababu ya majeraha ya misuli.



# Southgate bado ana watu







**LONDON,Uingereza**

MENEJA wa England Gareth Southgate ameongeza majina ya vijana watatu katika kikosi cha timu ya taifa kinachosaka tiketi ya kufuzu michuano ya Euro 2024. Vijana hao ni Cole Palmer, Ezri Konsa na Rico Lewis ambao wameitwa kwenye kikosi cha England kwa mara ya kwanza.

Kuongezwa kwa watatu hao kwa mechi mbili za kufuzu kwa Euro 2024 kunafuatia James Maddison, Callum Wilson na Lewis Dunk kujiondoa kwa sababu ya majeraha.

Mshambuliaji wa Chelsea Palmer na mlinzi wa Manchester City Lewis wamependishwa kutoka kwenye kikosi cha timu ya taifa ya England chini ya umri wa miaka 21 hadi kwenye kikosi cha wakubwa cha Gareth Southgate.Uingereza itacheza na Malta tarehe 17 Novemba na Macedonia Kaskazini tarehe 20 Novemba.

Kiungo wa kati wa Real Madrid Jude Bellingham hana shaka kwenye mechi hizo kwa sababu ya jeraha la bega.Wengi wa kikosi cha Gareth Southgate wanatakiwa kuripoti St George's Park siku ya Jumatatu na tathmini zaidi kufanyika," ilisema taarifa ya Uingereza.

Palmer, 21, alikuwa sehemu ya kikosi cha U21 cha England kilichotwaa Ubingwa wa Uropa msimu wa joto na amekuwa katika kiwango cha kuvutia Chelsea msimu huu. Alijiunga na The Blues kutoka Manchester City majira ya joto na kufunga penalti dhidi ya timu yake ya zamani katika sare ya 4-4 ya Ligi Kuu ya Uingereza Jumapili.

Lewis, 18, amekuwa akitajwa na Southgate mara nyingi na alikuwa sehemu ya kikosi cha City kilichoshinda Treble msimu uliopita.

Beki wa Aston Villa Konsa, 26, alishinda Kombe la Dunia la Vijana wasiozidi umri wa miaka 20 akiwa na England mnamo 2017 na ameisaidia timu yake kushika nafasi ya tano kwenye Ligi ya Premia msimu huu.

England tayari imefuzu kwa Ubingwa wa Ulaya huko Ujerumani Juni na Julai ijayo baada ya ushindi wa 3-1 dhidi ya Italia .

# Chelsea kama wameanza kujipata hivi

**LONDON, Uingereza**

KLABU ya Chelsea wameanza kuonekana kutoka katika hali ya ukame wa matokeo hadi katika kipindi cha neema hiki huku wakitoa ushahidi zaidi kwamba machipukizi ya urejesho wa vijana hatimaye yanachipuka vizuri chini ya uongozi wa meneja Mauricio Pochettino.

Ikiwa ushindi wa Jumatatu ya tarehe 6 wa 4-1 dhidi ya Tottenham utakumbukwa kwa Refa Msaidizi wa Video (VAR), kadi nyekundu, mabao yaliyokataliwa, ilikuwa ni mchezo kabambe , lakini pia sare ya jumapili dhidi ya Man City ya 4-4 ilikuwa ya kusisimua sana na kuwa kama sikukuu ya kandanda.





VAR, bila shaka, ilikuwa gumzo huko Stamford Bridge na zawadi ya penalti ya kipindi cha kwanza kwa City wakati Marc Cucurella alihukumiwa kuwa amemsukuma Erling Haaland uamuzi uliopingwa na msisitizo wa beki huyo wa Chelsea kwamba alichezewa vibaya kwanza.lakini pia mchezo uliamuliwa kwa penati ya mwisho aliyopiga Cole Palmer na kuwapa Chelsea alama moja muhimu.

Wakati huu, hata hivyo, vichwa vya habari lazima vidaiwe na ubora wa soka unaotolewa, mabadiliko ya bahati na ubora wa mchezaji mmoja mmoja.

Chelsea, haswa wameonyesha ari ya kutosha, nguvu za mwili na hisia kwa nusu msimu katika mechi zao mbili za mwisho za Ligi Kuu.

Chelsea na kocha Pochettino wamekuwa na wiki yao ya matukio mengi wakiwa pamoja tangu achukue usukani Julai lakini pia wiki yao bora zaidi wakiwa pamoja.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Novemba 15-21, 2023

# 5G sasa yawalewesha

Na Mwandishi Wetu

USHINDI wa mabao 5-1 dhidi ya mpinzani wao wa jadi, Simba ya Dar es Salaam sasa umeonekana kuanza kuwalevya mabingwa wa Tanzania Bara Yanga.

Yanga walizindua jezi zikiwa na matikeo hayo na majina ya wafungaji.

Katika wiki ya kushebherekea ushindi, Jumapili Yanga wakachinja ng'ombe ambao walitolewa na Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi, Paul Makonda kwa kila goli lililofungwa.



Yanga wakatangaza kuwa Jumapili ilikuwa siku ya kunywa supu makao makuu ya klabu hiyo.

Jana Jumanne saa 12.30 asubuhi Yanga wakadhihirisha wamelevya na ushindi huo baada ya kuzindua mabango kadhaa yenye mfano wa jezi ya mabao 5-1.

# Ulimwengu anasema halafu hasemi

Na Mwandishi Wetu

MSHAMBULIAJI wa Kimataifa wa Tanzania Thomas Ulimwengu amema klabu nyingi nchini hazithamini wachezaji wazawa badala yake inawekeza zaidi kwa wachezaji wa kigeni.

Ulimwengu ambaye kwa sasa anaichezea Singida Big Stars amesema wachezaji wa kitanzanua wana uwezo mzuri na vipaji vikubwa kuliko baadhi ya wachezaji wa kigeni wanaosajiliwa na klabu nchini.

"Mimi naona wachezaji wengi wamefanya (Tanzania) kama ni njia. Wanaona kabisa nikija Tanzania nikifunga magoli kadhaa naondoka. Hii ni kutokana na ushindani na nguvu ya mitandao ya kijamii," alisema.

Ulimwengu nyota wa zamani wa TP Mazembe amesema maslahi makubwa klabu za Tanzania zinatoa kwa wachezaji wa kigeni na hivyo kupelekea wachezaji wengi kuvutiwa kuja kucheza nchini.

"Hakuna mchezaji ambaye hapendi kwenda kwenye mpira akalipwa vizuri, wanakuja kwa sababu wanaona kuna mafanikio," amefafanua.

Ulimwengu amezitaka timu za Tanzania kuthamini wachezaji wazawa.



# Simba SC wao wahamisha vita

Na Mwandishi Wetu

KLABU ya Simba umeamua kuendelea kuhamimisha nguvu zake katika mitandao ya kijamii baada ya kuzindua whatsapp Channel ili taarifa zao kufikiwa na watu wengi zaidi

Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula amesema mjini Dar es Salaam kuwa klabu hiyi Instagram ina watu zaidi ya milioni 5.5, Facebook zaidi ya milioni 1.9 m, Twitter zaidi ya milioni 1.5 huku YouTube tukiwa na zaidi ya 438k wakati kwenye app imepakuliwa zaidi ya laki saba.

"Tunazindua Simba Sports Club WhatsApp channel. WhatsApp imepakuliwa na watu Bilioni 2.2 duniani ndio mtandao umepakuliwa zaidi duniani. WhatsApp wenyewe walitufata kuwa timu ya kwanza Afrika Mashariki na Kati kuwa na chaneli hii.

"Ni timu chache kama Kaizer Chiefs, Al Ahly, Barcelona, Real Madrid na Simba tumejiunga. Katika kuijaribu kabla ya kuzindua ndani ya wiki tumepata wafuasi laki moja. Faida kubwa ni mashabiki kupata taarifa na wadhamini wetu kuonyesha bidhaa zao."

Alisema chaneli pamoja na kutoa ajira lakini ni sehemu ya Wanasimba na watu wengine kupata taarifa sahihi za klabu. Hii ndio klabu ambayo inafanya vitu vyenye faida na tofauti.

**Tunazindua Simba Sports Club WhatsApp channel. WhatsApp imepakuliwa na watu Bilioni 2.2 duniani ndio mtandao...**

WhatsApp

# Barbara Loading ...



Na Mwandishi Wetu

WAKATI kukiwa na fukuto kubwa ndani ya timu ya Simba juu ya mambo mbalimbali ya Uongozi, aliyekuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara 'Babra' Gonzalez amestua ulimwengu wa wapenda soka nchini.

Babra ambaye alijiuzulu nafasi hiyo uko wakati ilionekana hawako vizuri na mwekezaji mkuu wa Simba, Mohamed Dewji kutoka kauli ambazo zilikuwa zikionekana kama majibizano katika mitandao ya kijamii.

Kabla ya kipigo cha mabao 5-1 kutoka kwa Yanga, asubuhi ya Jumapili Babra alitania kuwa Mvua na Simba ni kama wao ndio wanaongoza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na kuitakia heri timu yake.ww

Siku mbili baada ya kupigo hicho Babra alimtaka Admin wa mitandao ya kijamii kusitisha picha za pambano la 5-1 na kuangalia mechi zingine za mbele. Agizo ambalo lilitekelezwa.

Jana asubuhi Babra alipost picha akiwa kwenye kikao na Mo na huku akiandika Mabadiliko na Maendeleo huku 'akimtag' picha hiyo mwekezaji huyo.

Inaelezwa kuwa Babra amepewa majukumu na mwekezaji huyo katika kusaidia mambo ya utawala ikiwemo suala la kocha mpya.

Baada ya picha hiyo kusambaa, mashabiki wa Simba walieleza kummiss kiongozi huyo na kumtaka kurejea klabuni hapo akiwa kama Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi.